

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Nane – Tarehe 8 Novemba, 2007

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 101

Kituo cha Afya Mbwera

MHE. ABDUL J. MAROMBWA aliuliza:-

Kwa kuwa, ufunguzi wa kituo cha Afya Mbwera ulifanywa tarehe 27 Agosti, 1994 na aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wakati huo Mheshimiwa Dr. John Malecela, lakini hadi sasa kituo hicho hakina hadhi hiyo ya kuitwa kituo cha Afya:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni haja ya yeye Mwenyewe kwenda Mbwera kuona hali halisi ya kituo hicho badala ya kutoa taarifa ya simu kutoka kwa Wataalamu wake kuona kama kimekamilika?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha kituo hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa wazo la mimi kwenda Rufiji na kutembelea Zahanati ya Mbwera, nimelipokea na nitalifanyia kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Kimsingi ili Zahanati iwe kituo cha Afya ni lazima iwe na jengo la wagonjwa wa nje kwa ajili ya huduma za kawaida. Jengo kwa ajili ya kinamama wajawazito na jengo la utawala. Ni lazima pia ziwepo wodi mbili kwa ajili ya wanawake na wanaume, sehemu ya ufuaji, chumba cha maiti, na tanuru la kuchomea taka.

Kituo cha Afya pia kinahitaji kuwa na watumishi wa kada mbalimbali wapatao 29. ni kweli kuwa Zahanati ya Mbwera ni moja ya Vituo vya Huduma za Afya katika sehemu ya Delta Wilayani Rufiji. Kituo hiki kilianzishwa kama Zahanati na baada ya muda likajitokeza wazo la kupanua Zahanati hiyo kuwa kituo cha afya, na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ikaridhia wazo hili.

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo jitihada za kuongeza majengo zilianza, na hadi sasa nyumba tatu za watumishi zimejengwa, jengo la *OPD* limekarabatiwa na kupanuliwa, vitanda na vifaa vingine vimepelekwa na watumishi wameongezwa.

Aidha hivi sasa Zahanati imeanza kufanya kazi za kituo cha Afya kwa wagonjwa kupumzika. Juhudi za kuongeza watumishi kulingana na ikama kujaza nafasi zilizo wazi zinaendelea. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hiki kunategemea upatikanaji wa fedha za maendeleo pamoja na kuhamasisha Jamii kupitia mpango shirikishi utakaowezesha Jamii kuona umuhimu wa kuchangia gharama za upanuzi wa Zahanati hiyo ili kufikia hadhi ya kituo cha Afya.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kituo hiki cha afya kama nilivyozungumza mwanzoni kilifunguliwa na haikuwa zahanati. Mwanzoni ilikuwa ni zahanati lakini sasa hivi ni kituo cha afya kutokea mwaka 1994 na aliyekwenda kufungua kituo hiki ni Mheshimiwa John Samweli Malecela kule Mbwera. Je, Serikali haioni kuwa kwa kuwatumia viongozi wakubwa kufungua vituo kama hivi na kutovikamilisha kwa muda wa zaidi ya miaka 14 ni kumdhaliisha yule kiongozi aliyekwenda kufungua kituo hicho? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa, kituo cha afya Mbwera ndicho pekee kinachohudumia zaidi ya vijiji 18 katika delta ya mto Rufiji, na kwakuwa kituo hiki hakina gari, hakina mazingira ya kupeleka gari kwaajili ya kuwabebea wagonjwa. Je, serikali sasa ipo

tayari kutoa *ambulance* ya boti ili iweze kuwasafirisha wagonjwa kutoka Mbwera hadi Muhoro zaidi ya kilometa 50 ili waweze kufika Hospitali ya Rufaa ya Utete?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Mbwera haijakidhi kiwango cha kuitwa kituo cha afya ingawa imeanza kutoa huduma kwaajili ya matatizo yaliyopo katika mazingira yale. Jengo lililopo ni moja tu ambalo limewekewa *partition* kwa sehemu mbalimbali kwamba sehemu hii walazwe wagonjwa, sehemu nyingine wanapimwa wamama wajawazito, lakini haijakidhi hasa vile vigezo vya kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, pia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ya Rufiji ilipelekewa hela za ukarabati wa vituo vya afya shilingi milioni 150, na bado sasahivi milioni 50 hazijapwlekwa. Mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ione umuhimu wa kutumia fedha hizo katika kukipanua kituo hicho ili kiwe kituo cha afya kamili na sio Zahanati. Kwahiyo ningemwomba tu Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane ili kuhakikisha kwamba huduma za kituo cha afya zinafikiwa katika zahanati hiyo.

Kuhusu swali la pili, ni kweli kwamba eneo la Delta ni eneo ambalo kijiografia lina matatizo na vijiji ni vingi sana kutoka baharini na kuja katika sehemu moja ya Mbwera. Ninachoweza kusema kwamba Serikali kwa mwaka huu haijatenga fedha zozote kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa. Hapo Serikali itakapokuwa na hali nzuri na tutakapokuwa na bajeti ya kununua magari kwaajili ya kubebea wagonjwa, Rufiji ni mojawapo kati ya Wilaya ambazo zitafikiriwa hasa kwa eneo hili la Delta. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili bajeti ijayo tuone kwamba kama tutapangiwa kununua magari ya vituo vya afya

MHE. SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, alichokiomba Mheshimiwa Mbunge, ambacho nadhani na Waziri atayehusika atakizingatia ni chombo cha usafiri cha *ambulance* cha kupita kwenye maji, sio gari.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitoe maelezo ya ziada kidogo kuongezea pale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri, ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, kwanza tukubali kama Serikali kwamba eneo lile la Delta ni gumu na kwa kweli linahitaji kidogo *sympathy* ya Serikali. Suala hili la kituo cha Afya cha Mbwera ni la muda mrefu na nadhani kama Serikali ni wajibu wetu sasa kujaribu kuona ni juhudi zipi zinaweza zikawekwa kwa nguvu zaidi ili kuweza kwa kweli kupunguza ile kero ambayo kwa Delta ni kubwa sana.

Kwa hiyo nataka nimWombe tu Mheshimiwa Mbunge, avute subira kidogo tujaribu kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukachukua hatua za ku *speed up* ujenzi.

Lakini naomba vile vile nimWombe sana atuvumilie kidogo, suala hili la Mbwera kwa sababu ni *complicated*, ni kweli huwezi ukapeleka gari la wagonjwa. Lakini kinachohitajika ni boti, sasa *whether* itaitwa *ambulance* au kwanza tuanze na boti ya kawaida lakini nalo ni jambo ambalo awamu iliyopita tulijaribu kulifanyia kazi. Nataka nimhakikishie kwamba bado tunalishughulikia tutaona ni kitu gani kitajitokeza mwisho wa zoezi hili. Nakushukuru Mheshimiwa Spika.

Na. 102

Ujenzi wa Hospitali ya Kisasa – Serengeti

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Serengeti mwezi Septemba 2005 aliwaahidi wananchi kuwa Serikali itawajengea Hospitali ya kisasa:-

(a) Je, ni lini Serikali itanza ujenzi wa Hospitali hiyo, itagharimu kiasi gani na kazi hiyo itamalizika lini?

(b) Je, ujenzi wa Hospitali hiyo utagharimu fedha kiasi gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wanyancha Mbunge wa Serengeti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma bora kwa kila Mtanzania zinatolewa. Na hivi sasa Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais, zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais, alipotembelea wananchi wa wilaya ya Serengeti mwaka 2005 aliwaahidi kuwajengea hospitali ya kisasa. Mikakati ya kutekeleza ahadi hii tayari imekwisha anza kwa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwa kushirikisha wananchi wake kupitia vikao mbalimbali kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, wilaya na hatimaye kupata baraka katika kikao cha ushauri cha Mkoa wa Mara yaaani *RCC*.

Mheshimiwa Spika, aidha hatua mbalimbali za kuanza ujenzi zimekwishafikiwa ikiwa pamoja na kutenga eneo lenye ukubwa wa ekari 40 ambapo ekari 20 zimetolewa na

wananchi wa wanakijiji cha Matare na ekari nyingine 20 zimetolewa na wakazi wa kijiji cha Kibeyo.

Eneo hili lililotengwa liko umbali wa kilometa 5 kutoka Mugumu mjini na kilometa 7 kutoka hospitali ya Kanisa ya *MenoniteTanzania*. Tayari Wataalamu kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na pia Wataalamu wa fani ya Usanifu Ardhi toka ngazi ya Mkoa na Wizra ya Ardhi, walishafika katika eneo lililotengwa na kufanya utafiti katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha Halmashauri kwa kutumia kampuni ya ujenzi ya *MDL* ya Dar es Salaam, imekwisha andaa michoro ya Hospitali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali hii unatarajiwa kugharimiwa na wananchi wa Wilaya ya Serengeti na pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo na Serikali kuu. Kulingana na taarifa za Mthamini wa Majengo, Hospitali hiyo itagharimu shilingi bilioni 11 fedha za Kitanzania.

Hadi sasa Serikali Kuu imekwishatoa shilingi milioni 200 na Halmashauri ya wilaya ya Serengeti imetenga shilingi milioni 70 katika bajeti ya mwaka huu wa 2007/2008 Mheshimiwa Spika, aidha Halmashauri itaendelea kutenga fedha za ujenzi huo katika bajeti zijazo na pia inaendelea kuwashawishi wahisani katika kuchangia ujenzi huo.

Ni matarajio yetu kuwa ujenzi rasmi wa hospitali hii utanza mara tu Wataalamu wa Ardhi na Afya watakapokamilisha taarifa yao na Wizara ya Afya kutoa kibali cha ujenzi.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza Wilaya ya Serengeti ina kilometa za mraba 10,300 lakini ina vituo viwili tu vya afya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea vituo vya afya ili kuondoa kero za wananchi kutembea umbali mrefu ili kupata matibabu ?

Mheshimiwa Spika, pili, Hospitali tuliyonayo ya *Nyerere DDH* ya sasa na vituo vya afya vina upungufu mkubwa wa waganga na vifaa. Je, serikali ina mpango gani wa kuboresha hiyo haspitali pamoja na vituo hivyo viwili vya Afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kweli Wilaya ya Serengeti ina kilometa za mraba 10,300 na ni keli nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ina vituo vya afya ni viwili tu. Lakini Mheshimiwa Mbunge,

anafahamu kabisa kwamba serikali ina mpango wa kujenga vituo vya afya katika kila kata na zahanati kwa kila kijiji. Kwahiyo mpango huu kwakuwa utakuwa umeendeshwa Tanzania nzima kuanzia mwaka wa 2008/2009 na Serengeti ni mojawapo, kwahiyo huo ni mpango kabambe wa Serikali ili kuhakikisha kwamba huduma za afya zinatolewa katika kila kijiji na katika kila kata.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa watumishi kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka huu Wizara ya Afya imeongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vyake na pia imetanua na kufungua vyuo mbalimbali vya afya ili kukidhi mahitaji ya watumishi wa afya, uhaba wa watumishi wa afya ni mkubwa na sio kwa Serengeti peke yake bali ni kwa Tanzania nzima. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, watumishi hao watakapo, hao wanafunzi wakikamilisha masomo yao watapangiwa moja kwa moja kwenye Wilaya mbalimbali.

Na. 103

Huduma za Afya Geita

MHE. ERNEST G. MABINA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Geita kwa sasa inakadiriwa kuwa na jumla ya watu 810, 548 kati yao wanaume wakiwa 404, 735 na wanawake 405,813 ambao ni ongezeko la asilimia 3.4 na kwa kuwa idadi hiyo kubwa ya watu inahudumiwa na hospitali moja ya Wilaya, vituo vinane (8) vya Afya, Zahanati 44 na ina gari moja tu la kubeba wagonjwa ambalo ni bovu:-

(a) Je, Serikali inaona huo ni uwiano mzuri wa kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Geita?

(b) Je, ni lini Serikali italeti magari ya kubeba wagonjwa kulingana na hali halisi ya Wilaya ya Geita?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali halisi ya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi wa Wilaya ya Geita kuwa si za kuridhisha. Kulingana na idadi ya watu waliopo Wilayani Geita ambayo inakadiriwa kuwa ni watu 810,543 Wilaya inatakiwa kuwa na Hospitali tatu, vituo vya afya 16 na zahanati 81. Kwa sasa Wilaya ina Hospitali moja, vituo vya afya vinane na zahanati 51.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona upungufu huu imeanzisha mikakati ya makusudi ya kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa Wilaya ya Geita. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kupandisha hadhi vituo vya Afya viwili kuwa Hospitali. Vituo hivyo ni pamoja na kituo cha Afya cha Karumwa katika Tarafa ya Msalala ambapo tayari huduma za upasuaji zimeanza kutolewa. Pia kituo cha afya cha Katoro katika tarafa ya Butundwe ambapo kiko kwenye mkakati wa kupandishwa hadhi kuwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kupitia mpango wa *TASAF II* imeanza kujenga zahanati 6 katika vijiji vya Lyulu, Kitongo, Ndelema, Buyagi, Msasa pamoja na Ibondo. Ujenzi wa zahanati hizi unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita inalo gari moja la kubebea wagonjwa ambalo lilikuwa bovu. Ubovu wa gari hilo ulitokana na ukosefu wa vipuri hapa nchini, vipuri hivyo vinapatikana nchini Korea Kusini, ambako gari hili lilitengenezwa.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba vipuri vimeagizwa nchini Korea Kusini na vimekwisha patikana na gari hilo liko kwenye matengenezo Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Bungeni namba 185 la Mheshimiwa Msalika, Mbunge wa Nyanghwale, kwenye Mkutano wa nane wa Bunge lako Tukufu tarehe 9 Julai, 2007, nilieleza juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya Wilayani Geita, ni pamoja na suala la ununuzi wa magari mawili ya kubebea wagonjwa. Halmashauri ya Wilaya ya Geita katika Bajeti yake ya mwaka huu 2007/2008 imetenga fedha kwaajili ya kununua gari moja la wagonjwa litakalotumika katika kituo cha afya cha Karumwa.

Aidha kupitia maombi maalum yaliyowasilishwa Hazina, Halmashauri iliidhinisha Bajeti ya kununua gari lingine, hadi sasa hatua za manunuzi zimeshafanyika na magari yote mawili yameshalipwa fedha kiasi cha shilingi milioni 150 kwa kampuni ya *Toyota Tanzania Ltd.*

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nieleze tu tatizo kubwa la Geita ni kwa sababu ya ukubwa wa Geita na wingi wa watu kwa jinsi Geita ilivyo. Geita kulingana na idadi ya watu na ukubwa wake inakaribia sana Mkoa wa Singida, inakaribia sana Mkoa wa Lindi na inakaribia kidogo nchi ya Zanzibar. Sasa huduma inayozipata ni za Kiwilaya.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa serikali ifikirie sasa Geita kuilea kama Mkoa ili iweze kupata huduma za kimkoa ikiweza kwa kuangalia idadi ya watu ilionao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rwilomba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Wilaya hiyo ni kubwa na hata idadi ya wakazi wake ni kubwa. Hasa anachoomba ni uwezekano wa kuwa wilaya hiyo sasa ifikiriwe kuwa Mkoa. Labda niseme waziwazi tu kwamba haitawezekana kwa maana ya Wilaya kuwa Mkoa.

Lakini Mheshimiwa Spika, tulishawaandikia wenzetu wa Mkoa wa Mwanza, Shinyanga na Kagera tukaomba wakae pamoja waangalie uwezekano wa kuwa na wilaya mbili tatu ambazo zinapakana mipaka katika juhudi za Serikali kujaribu kusogeza uongozi karibu zaidi na wananchi ili kama masharti yale yatakidhiwa vizuri basi eneo hilo lingeweza likaunda mkoa mpya kati ya mikoa hiyo mitatu.

Kwa hiyo, labda nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Wabunge wetu wa mikoa yote mitatu na uongozi wa Mwanza, basi waendeleze hizo juhudi wakamilishe watuletee. Na mimi ninaamini wilaya ya Geita itakuwa ni moja kati ya wilaya hizo zinazofikiriwa.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba katika swali langu 187 nimeuliza Serikali iliahidi kwamba Halmashauri imetenga pesa kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo cha afya cha Kalumwa. Na kwa kuwa, Kalumwa kuna wagonjwa wengi na wanahitaji kupelekwa hospitali za rufaa za Geita, Mwanza, Sengerema na sehemu nyingine. Na kwa kuwa, wamekuwa wakisubiri sana gari lile kama vile watu walivyokuwa wanamsubiri Masiha siku za nyuma. Je, ni lini gari hilo litafika sasa Nyangh'wale, Msalala?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeshasema kwamba, fedha zimeshalipwa kwenye kampuni ya *Toyota Tanzania Ltd.* Ina maana kwamba mchakato umeishakwisha, fedha tumeishalipwa na wakati wowote gari hilo litakuwa limefika. Kwahiyo, wananchi wa Karumwa wawe na subira kwamba gari litapatikana hivi karibuni na si muda mrefu.

Kuimarisha Usafiri wa Reli

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa, usafiri wa reli ni kiungo cha Wilaya ya Mpanda na sehemu nyingine nchini na unategemewa kwa kusafirisha abiria na mizigo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuimarisha njia ya reli, kuongeza mabehewa kwa wasafiri wa madaraja yote na vichwa vya treni (*engines*) ambazo zimekuwa zikiharibika mara kwa mara?
- (b) Je, ubora wa huduma, usafi na taa katika mabehewa utaboreshwa lini?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye Sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, serikali inayo mipango ya muda mfupi na muda mrefu inayolenga katika kuimarisha njia, mabehewa na vichwa vya treni kama ifuatavyo:-

Mipango ya muda mfupi ni kama ifuatavyo:-

(i) Benki ya Dunia imetoa mkopo wa milioni 33 dola kwa Serikali yetu kwa ajili ya kutengeneza kilometa 197 kwenye sehemu mbalimbali za reli ya kati kawa kubadilisha reli zilizochakaa na kuweka mpya za uzito wa paundi 80 kwa yadi kama ifuatavyo:-

Kintinku-Makutupora	16	kms
Itigi-Malongwe	105	kms
Igalula	-Tabora	37 kms
Tabora	-Mabama	39 kms

Jumla 197 kms

(ii) Kujenga vituo vya kuhudumia makontena (*Container Depots*) Ilala, Shinyanga na Mwanza kwa ufadhili wa pamoja kati ya Serikali ya Ubelgiji na Serikali ya Tanzania.

(iii) Kukarabati njia kilometa 26.5 kati ya Tabora na Kigoma kwa kubadili reli zilizochoka na kuweka reli imara.

(iv) Kuendelea kuboresha reli za Kaliua – Mpanda na Manyoni – Singida.

(v) Miundombinu ya mawasiliano kupitia mradi wa *Telecommunication Network phase III* (Dodoma Tabora). Mradi huu ulikamilika mwaka 2006 na hivi sasa zinatafutwa fedha za kutandika nyaya kati ya Tabora – Kigoma na Tabora – Mwanza.

(a) Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha huduma za Shirika la Reli Tanzania, Serikali imekodisha huduma hizo kwa muwekezaji binafsi kwa kipindi cha miaka 25 kuanzia Septemba 2007. Katika kipindi hicho reli hii inatakiwa kuboreshwa kufikia uzito wa ratili 120 kwa yadi ili uweze kuendana na maendeleo ya reli duniani na kutoa huduma bora.

Katika kipindi hicho muwekezaji kwa kushirikiana na Serikali anatarajia kuboresha hali ya miundombinu. Ki mkataba muwekezaji anatarajiwa kukarabati kilometa 648 za reli ya kati kwa kutandika reli za uzito wa ratili 80 kwa yadi na sehemu nyingine ya njia iliyobaki itashughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali itabidi iongeze sehemu ya gharama ili uboreshwaji ufikie ratili 120 kwa yadi. Aidha muwekezaji anatarajiwa kuongeza sehemu ya gharama ili kuboresha huduma kwa kukarabati mabehewa na vichwa vya treni na kuongeza vingine kufuatana na mahitaji yatakavyokuwa yanajitokeza.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ilipokuwa ikiandaa taratibu za kukabidhi uendeshaji wa Shirika kwa Mkodishaji, shirika lilijitahidi kuboresha huduma zake na kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa kufanya matengenezo ya njia, mabehewa, injini na taa kwenye mabehewa ya abiria licha ya kuwa na hali ngumu ya kifedha.

MHE. MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika mpango mfupi wa utengenezaji wa reli amezungumzia kuhusu kutengenezwa kwa reli ya kati na meneo ambayo kama alivyokuwa ameyataja na akasema kwamba reli kutoka Kaliuwa kwenda Mpanda yenyewe imo katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kujua hasa ni eneo gani ambalo litakaloshughulikiwa kama alivyokuwa ameanisha katika reli ya kati maeneo mbalimbali?

Swali la pili, kwa kuwa maswali yanachukua muda mrefu kujibiwa na hatimaye shirika la reli sasa hivi linaendeshwa na kampuni ya *Rights* pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nilikuwa nataka kusikia kauli ya Serikali kwamba kampuni hii mpya itahusika katika uendeshaji wa njia ya Kaliuwa Mpanda na Manyoni Singida?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi kama, ifuatavyo:-

La kwanza, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba reli ya Kaliuwa Mpanda itatengenezwa kwa kubadilisha reli zilizopo na kuweka reli za paundi 80 kwa yadi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri jana wakati akijibu hoja mbalimbali za hapa Bungeni. (*Makofi*)

Kazi hiyo itafanyika ikiwa ni pamoja na Manyoni Singida, kwa sababu zile zilizoko ni za pauni 56.

Hiyo itafanyika ikiwa ni pamoja na Manyoni – Singida kwa sababu zile zilizoko ni pauni 56. Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba uendeshaji ambao amepewa mwekezaji shughuli hizi zimeshaanza rasmi na zinaendelea vizuri kwa mtandao mzima wa reli. (*Makofi*)

Pale ambapo tunahisi huduma kama Kaliwa – Mpanda na Manyoni – Singida kwamba hazitaleta faida Serikali itabidi ifidie katika kutoa huduma katika maeneo hayo mawili.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba kuuliza swali moja tu.

Je, ni sababu zipi zilizosababisha kusitishwa kwa safari za kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na kama ni ubovu wa reli. Je, reli hiyo imeshatengezwa na mbona watu wanalamika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI): Mheshimiwa Spika, huduma za reli ya kati zilisitishwa na zikaanzia Dodoma kutokana na ukosefu wa injini za kutosha na mabehewa. Lakini pia, kuna matatizo ya njia ya reli ambayo kama nilivyoeleza hapo mwanzoni mikakati yote imepangwa kwa ajili ya kushughulikia shughuli hizi.

Lakini napenda nimhakikishe Mheshimiwa Genzabuke kwamba mwendeshaji tumemkabidhi juzi tu hata kama tungetaka afanye maajabu ya kupata *engine* mpya na mabehewa mapya si rahisi kwa sababu ni lazima yaundwe huko yanakoundwa na kuletwa hapa.

Tumpe muda tuone anafanyaje kwa sababu tunao muda wa kufanya *review* na yeye kila baada ya miaka mitano kujua amefanya nini na kipi hakikufanyika na nani ana wajibu wa nini. Namwomba Mheshimiwa Genzabuke awe na subira. (*Makofi*)

Na. 105

Nyumba Zilizowekewa Alama X

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kwa nyumba zilizowekewa alama X tangu mwaka 2003 lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea tangu muda huo?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nyakayamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara sura ya 167 iliyotungwa mwaka 1932 na kufanyiwa marekebisho ya mara kadhaa na sheria mpya ya barabara (*Road Act 2007*) ambayo imeanza kutumika baada ya kuridhiwa na Mheshimiwa Rais, zinakataza mtu yeyote kufanya maendelezo aina yoyote kwenye hifadhi ya barabara kuu, Barabara za Mkoa na za Wilaya. Eneo la hifadhi ya barabara lililoainishwa kisheria ni kama ifuatavyo:-

1. Karibu barabara zote kuu na barabara za Mkoa hifadhi ya barabara ni futi 75 ama meta 22.86 kila upande kuanzia katikati ya barabara.

2. Barabara za Wilaya hifadhi ya barabara ya ni futi 33 (mita 10.06) kila upande wa barabara kuanzia katikati ya barabara.

Mheshimiwa Spika, sheria ya barabara inatoa uwezo kwa mamlaka yenye dhamana ya barabara kutoa notisi ya kukataza maendeleo ya aina yoyote ndani ya hifadhi ya barabara na kwamba kukaidi notisi iliyotolewa, mamlaka husika ina uwezo wa kuingia na kuondoa maendeleo hayo kwenye hifadhi ya barabara kwa gharama ya mhusika.

Kutokana na sheria hii, Wizara ya Miundombinu imekuwa ikiwatahadharisha wananchi wote waliojenga ndani ya hifadhi ya barabara kwa kuwawekea alama X mapema hata kama hakuna mpango wa siku za karibuni kujenga/kupanua barabara husika ili wajue kuwa kuna siku watapaswa kuondoka kwenye eneo hilo wakati wa upanuzi, ujenzi na matengenezo ya barabara yatakapotakiwa kufanyika.

Hata hivyo kwa maeneo mengine ambapo hivi sasa Serikali haina mkakati wowote wa ujenzi wa barabara, nyumba zote zilizowekewa alama ya X ni ishara ya kuwatahadharisha wananchi wanaohusika kuwa hapo walipo siyo sahihi hivyo wasifanye maendeleo zaidi na kwa kweli waanze kwa hiari yao kuondoa mali zao ndani ya hifadhi ya barabara ili kuepuka usumbufu siku zijazo.

Ningependa kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, wasaidie kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuepuka kujenga ndani ya eneo la hifadhi ya barabara kwani eneo hili limetengwa mahsusi kwa ajili ya matumizi ya barabara.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ipo dhana ya kwamba kuna watu ambao wamekwishajenga kabla ya barabara kupita. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwabaini wale ambao barabara imewakuta na hiyo Serikali inachukua hatua gani? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sheria ya barabara ya mwaka 1932, sheria hiyo ilipotungwa mwaka huo alikuwepo kwenye eneo hilo anastahili fidia kama eneo lake litatumika kwa ajili ya barabara.

Kwa kuthibitisha hilo kuna njia nyingi na yeye yuko kwenye eneo hilo, hutoa uthibitisho na Serikali vile vile kwa kuangalia vithibitisho mbalimbali huweza kugundua kwamba kweli huyo mtu alikuwepo kabla ya sheria hiyo kutungwa.

Kwa hiyo, yote hayo yeye mwenyewe analeta ushahidi na vile vile Serikali inafanya utafiti kuangalia kama kweli alikuwepo katika eneo hilo. Lakini kama amejenga baada ya sheria hiyo kupitishwa yaani baada ya mwaka 1932 ni kwamba sheria inasema hastahili kulipwa fidia yoyote. (*Makofi*)

MHE. MANJU S. O. MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kufuatia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, eneo la barabara kutoka Simbo hadi Uvinza wa kazi wamekwenda pale mwaka 1974 wakati wa *operation*. Kwa hiyo, ni dhahiri kulikuwa hakuna barabara.

Lakini nyumba zimetwa X na Mheshimiwa Naibu ana kumbukumbu nzuri ulikuja ujumbe wakati wa kikao cha Bajeti mwaka jana kuja kumwona. Sasa eneo hili ambalo wananchi walijenga kabla barabara haijakuwepo, hivi hawa wananchi wanatakiwa walete udhibitisho gani wakati Serikali inatambua iliwakuta wananchi na ikajenga barabara wakati wananchi wakiwa wako pale? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema sheria inayohusika ni ya mwaka 1932 na kama sheria hiyo ilikuwa inaainisha wakati ule kwa sababu ilitoa *schedule* ya

barabara kwamba kulikuwa na barabara kati ya Simbo na Uvinza wakati huo basi ina maana kwamba barabara ilikuwepo na kama wananchi walihamia mwaka 1974 ina maana wananchi ndio walioingia kwenye eneo la barabara.

Hata hivyo Serikali inafanya utafiti mbalimbali na kuona kwamba je, hawa wananchi ile barabara ilikuja kupinda kuingia kwenye eneo lao au wao ndiyo wameingia kwenye eneo la barabara. Ni kweli kwamba alileta wananchi ambao tuliona na suala hili linaendelea kushughulikiwa ili kuona haki kwa sababu kwa kweli Serikali ina nia ya kufanya haki pale ambapo haki inastahili kutendeka.

Na. 106

Barabara ya Mikumi Kilosa

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa, mwezi Agosti, 2006 aliyekuwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha walipotembelea barabara ya Mikumi – Kilosa, wakiambatana na Mbunge wa Mikumi, walishuhudia na kuridhia umuhimu wa kiuchumi wa barabara hiyo ambayo imepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya Mwaka 2005 kwamba, gharama za ujenzi wa madaraja manne (4) ya *feeder roads* zinazovuka mto Miyombo unaoambaa ambaa na barabara hiyo katika Kata za Ulaya na Zombo zijumlishwe katika mradi mzima:-

Je, Serikali imelizingatia jambo hilo katika *survey* ya awali iliyofanyika ili lengo lisije likasahaulika katika mradi huo.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mikumi – Kilosa (km.78) ni sehemu ya barabara ya Mikumi – Kilosa – Dumila – Magole – Mziha – Handeni – Korogwe yenye urefu wa jumla ya kilometa 434. Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa sehemu ya Mikumi – Kilosa hadi Dumila (km. 146) umekamilika.

Ni kweli wakati wa ziara ya Waziri wa Miundombinu Wilaya ya Kilosa akifuatana na Naibu Waziri wa Fedha iliyofanyika mwezi Agosti 2006 yaliyotolewa maombi ya kuyaingiza madaraja manne (4) yaliyo katika barabara ya Wilaya (*Distric Road*) katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliyachukua maombi hayo ili kuyafanyia kazi. Hata hivyo kwa kuwa wakati maombi haya yanatolewa mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa sehemu ya barabara hiyo ambako yako madaraja hayo, alikuwa amepatikana na kuanza kazi kwa kufuata hadidu za rejea zilizomo katika mkataba, ilionekana ni vyema mhandisi mshauri akaendelea na kazi kwa mujibu wa mkataba wake. Madaraja hayo manne yataingizwa kwenye mradi katika hatua ya usanifu kamili (*detailed design*).

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kila panapojengwa barabara mpya ni busara na hekima barabara mpya iwafuate watu na siyo kuwakimbia, hasa kama watu wale katika maeneo inapopita ni wakulima wanaozalisha mazao ya biashara kwa wingi na chakula ili kuinua uchumi. Je, Serikali iko tayari kufikiria barabara hii baada ya kupita Zombo ipite jirani na Kijiji cha Kilangali ambako Serikali imegharamia kwa fedha nyingi sana mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji wa zao la mpunga na ambapo kuna uwezekano wa kulima mara mbili kwa mwaka hekta 1200 lakini tatizo lao kubwa ni usafiri wa kutoa mazao hayo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kama unavyosema ni vizuri barabara ikafuata watu. Lakini uzoefu pia unaonyesha kwamba watu hufuata barabara mpya. Lakini kuhusu swali lake ni kwamba tathimini ya kimazingira na kiuchumi inapofanyika wakati wa *survey* na wakati wa kufanya upembezi yakinifu mambo yote ya kiuchumi na kimazingira huangaliwa. Sasa pale ambapo washauri wa kitaalaam wanaeleza kwamba barabara hii ifuate mkono huu ina maana kwamba hayo yote yamezingatiwa. Ndiyo maana tunawapa watalaam watuelezee ni namna gani barabara inaweza kupita ili mambo yote haya ya kiuchumi na ya kimazingira na mengine yaweze kuangaliwa.

Kwa hiyo, mimi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tumefuata ushauri wa kitalaam na kwa kweli maeneo mengi tu yana umuhimu wa kiuchumi. Sasa barabara haiwezi kuwa inapindapinda tu kufuata maeneo ya kiuchumi, ya kilimo na kadhalika. Bila kuangalia vile vile maslahi mengine au mambo mengine ambayo yanatakiwa kwa msingi wa kitalaam kwenye masuala haya ya barabara. (*Makofi*)

Na. 107

Polisi Kuwapiga Watuhumiwa

MHE. JUMA H. KILIMBAH aliuliza:-

Kwa kuwa, wajibu wa polisi ni kulinda raia na mali zao; na kwa kuwa Jeshi la Polisi linaheshimika sana na kuthaminiwa na jamii ya Watanzania lakini sasa Polisi wametumia mwanya huo kwa kutumia madaraka yao vibaya pale wanapowapiga na kuwatukana matusi watuhumiwa wanapowakamata:-

(a) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa dhidi ya askari wanaofanya vitendo hivyo ambavyo ni makosa na vinakiuka haki za binadamu?

(b) Kwa kuwa, mara nyingi ipo tabia ya kulindana kwa askari hao pale raia anapoeleza juu ya unyanyasaji aliotendewa na askari wakati akimkamata kwa msemo kwamba uongo wa polisi sio kweli wa raia. Je, Serikali inayotaarifa ya jambo hili na kama ndivyo. Je, ni hatua zipi zimechuliwa dhidi ya tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, endapo Askari yeyote wa cheo chochote atagundulika kufanya kazi kwa kukiuka taratibu na maadili yake ya kazi ikiwemo kukiuka haki za binadamu atachukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na kanuni za kudumu za jeshi la polisi (*PGO*) na *Police Force Service Regulations* toleo la mwaka 1995. Askari huyo atashitakiwa kijeshi na kama atapatikana na hatia atapewa adhabu stahili ikiwemo kufukuzwa kazi kwa fedheha na wakati mwingine kufikishwa mahakamani kulingana na aina ya makosa aliyoshtakiwa kutenda.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya askari kama walivyo watumishi wengine wana tabia ya kutumia madaraka waliyopewa vibaya. Kutokana na kulitambua hili Serikali imeunda Idara ya Ufuatiliaji Usalama wa Raia katika Wizara ya Usalama wa Raia ambayo jukumu lake la msingi ni kusikiliza malalamiko ya wananchi na askari wenyewe dhidi ya utendaji wa jeshi la polisi. Aidha, Jeshi la Polisi limeunda chombo kiitwacho *Police Public Complaints (PPC)* kinachofanya kazi kwa kushirikana na idara hiyo mpya.

Hivyo basi raia yeyote anayeona kwamba hajatendewa haki na Askari Polisi wa cheo chochote ana uhuru wa kupeleka malalamiko katika idara ya ufuatiliaji au kitengo cha kusikiliza malalamiko katika jeshi la polisi. (*Makofi*)

MHE. JUMA H. KILIMBAH: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mawili ya nyongeza. Hawa polisi wa aina hii niliyowataja ni wajanja sana na hasa pale wanapogundua wewe raia waliyokufanyia makosa wakigundua kwamba una nia sasa ya kuchukua hatua dhidi yao basi wanakung'ang'ania wanakuchukua moja kwa moja mpaka kituoni na wanakufungulia mashitaka na wanakufungulia mashitaka kwa kukumbambikizia kesi.

(a) Je, Wizara inayo taarifa na kama inayo taarifa hii inawalinda vipi raia wa aina hii wanaotendewa makosa?

(b) Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie ni taratibu zipi zinazochukuliwa taratibu za kufaa za kuchunguza na kufuatilia nyendo za utendaji kazi za polisi hasa kimaadili utekelezaji wa maadili wa kazi zao.

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi wako askari ambao wakati mwingine maadili ya kazi zao, Serikali inafahamu kwamba wako askari wanaotenda vitendo viovu na ndio maana kwa makusudi kabisa Serikali kupitia Wizara ya Usalama wa Raia cha ufuatiliaji katika suala zima la usalama wa raia ili kuona wale wanaofanya makosa hatua zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuthibitisha hayo hivi sasa askari 28 wameshafukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali ilipoanzishwa idara hiyo. Hivyo napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu uliopo upo wa uhakika kwa wale wote wanaofanya makosa na wanapogundulika.

Kuhusu swali la pili kuendelea kufanya uchunguzi wa kina kama nilivyosema kwamba kwa kuwa idara hiyo ya ufuatiliaji ipo basi namhakikisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba utaratibu ni mzuri na wale wote ambao wanatenda makosa watachukuliwa hatua. Na kama nilivyosema kwamba kwa sababu idara hiyo zipo basi wananchi wapeleke malalamiko yao kwa nia ya kuyashughulikia ili waondolewe matatizo hayo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Nakushukuru kwa kuniruhusu swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Jeshi la Polisi wanapofanya vitendo vinavyokiuka haki za binadamu wanachukulia hatua. Je, ni hatua gani zilichukuliwa kwa polisi ambao waliwapiga marungu hadharani katika mji wa darajani Ugunja, mwaka 2000 wananchi ambao hawana hatia tendo ambalo lilikuwa linaonyeshwa mara kwa mara na televisheni za ndani na nje ikiwemo *CNN*.

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu yaliyotangulia kwamba askari wote wanaofanya makosa ya kupiga raia wema basi wanachukuliwa hatua zifaazo. Kwa hiyo, lazima tuelewe kwamba pia askari wanawajibu wa kufanya kazi pale raia wanapofanya vurugu. Kwa hiyo, inatazama nani alifanya makosa yule aliyeonekana amefanya makosa ndiye hatua zinachukuliwa juu yake. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina habari kwamba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed hayupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Abubakary swali linalofuata.

Na. 108

Kesi zinazoihusu Serikali

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (K.n.y. HAMAD RASHID MOHAMED) aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Serikali inaweza kushitaki au kushitakiwa:-

- (a) Je, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2007 Serikali ilikuwa na kesi ngapi imeshitakiwa na kati ya hizo, Serikali imeshinda kesi ngapi na imeshindwa kesi ngapi?
- (b) Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwa kesi ambazo imeshinda na kiasi gani kwa kesi ambazo imeshindwa?
- (c) Kwa mujibu wa Sheria. Je, Wakili anayekodishwa na Serikali hutakiwa alipwe asilimia ngapi kwa kila shauri analolisimamia Mahakamani?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA lijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, napenda kutoa maelezo ya jumla yafuatayo:-

Ni kweli kwamba Katiba pamoja na sheria za nchi zinaruhusu Serikali kuweza kufunguliwa mashauri ya madai Mahakamani. Kesi za Serikali au dhidi ya Serikali hutakiwa kufunguliwa katika Mahakama Kuu. Mbali na mashauri ya madai ya kawaida, yapo mashauri mengine kama yale yanayohusu wananchi kupinga maamuzi yanayofanywa na mamlaka mbalimbali (*Prerogative Orders*). Hayo hufuata taratibu tofauti. Aidha, yapo mashauri ya upatanishi (*Arbitration*) ambayo hutokana na mikataba. Haya hushughulikiwa kwa kufuata maelewano yaliyofikiwa katika mikataba husika.

Baada ya maelezo hayo ya jumla, napenda sasa kujibu sehemu (a), (b) na (c) za swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2000 na Septemba, 2007 Serikali ilikuwa mhusika katika mashauri ya madai ya kawaida na maombi ya kupinga maamuzi ya mamlaka mbalimbali 4,381 ambapo katika mashauri 54 ilikuwa mdai na katika mashauri 4,227 ilikuwa mdaiwa. Kati ya kesi hizo, kesi 2,327 zilitolewa maamuzi ambapo ilishinda katika kesi 1,927 na kushindwa katika kesi 400 tu.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kesi za kawaida na kesi za maombi ya kupinga maamuzi ya mamlaka mbalimbali, Serikali huwatumia mawakili wa Serikali ambao ni waajiriwa kwa ajili ya kuendesha kesi hizo. Mawakaili hawa hulipwa mishahara kama watumishi wa Serikali na kwa mishahara huo, hufanya kazi nyingine zaidi ya zile za kuiwakilisha Serikali Mahakamani. Hivyo ni vigumu kutoa mchanganuo wa kujua kiasi ambacho kimetumika katika kesi ilizoshindwa na kipi katika kesi ilizoshinda.

Aidha, napenda kuchukua fulsa hii kuwapongeza mawakili wa Serikali kwa kazi zao nzuri sana wanazozifanya licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo hivi sasa tunajitahidi kuyaboresha.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mashauri ya kawaida Serikali hutumia mawakili wake na kama ilivyokwisha kuelezwa hulipwa mishahara kama watumishi wa Serikali. Hivyo hakuna kiwango maalum cha malipo wanayopewa kwa ajili ya kesi ambazo wakili huyo amewakilisha. Hali hiyo ni tofauti na mawakili wa binafsi ambao hustahili kulipwa kiwango kinachoweza kufikia asilimia 3 ya madai yanayohusika mahakamani. Kwa upande wa mashauri ya upatanish (*Arbitration*) ambayo ndiyo huweza kuhusisha Serikali kutumika Mawakili binafsi, haya hushughulikiwa kwa kuzingatia mkataba. Hivyo hata upande wa malipo, huzingatia mkataba unaotengenezwa baina ya Wizara husika ya Serikali na hao mawakili. Hakuna asilimia maalum ambayo imepangwa kwa huduma hiyo.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza kwa sababu Serikali ina mawakili wa Serikali na wakati kesi zinapokuja za *arbitration* ni kwa sababu wanatumia mawakili wasiokuwa wa Serikali wakati wa mawakili wa Serikali wapo?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ulazimika wakati mwingine kuajiri au kuwataka mawakili binafsi kuiwakilisha katika za *arbitration* na sababu kubwa ni kwamba *arbitration* inataka utaalum maalum na ni watu wachache sana katika nchi yetu kwa mfano ambao wana kile cheti kinachotolewa chombo cha *arbitration* cha kimataifa kuwatambua kama ni *arbitrators*. Humu ndani nafikiri yumo Mheshimiwa Marmo peke yake ambaye ndiyo ana cheti kama hicho. Kwa hiyo, ni utaalum ambao bahati mbaya bado tunawa-*train* watu wetu waupate. Tunalazimika kuajiri wale ambao tayari wanao.

Na. 109

Ujenzi wa Madarasa na Nyumba za Walimu Nzega

MHE. LUCAS L. SELELII aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Wilaya ya Nzega wamehamasika katika kuchangia ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu; na kwa kuwa katika Jimbo hilo yapo maboma mengi yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na fedha za kukamilisha majengo hayo hazijatumiwa:-

- (a) Je, ni lini fedha za MEM zitatumiwa ili kukamilisha majengo hayo?
- (b) Je, Serikalil haioni kuwa kuchelewesha fedha hizo ni kuwakatisha tamaa wananchi wa Nzega?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara inafahamu kuwa hadi Septemba, 2007 Wilaya ya Nzega ilikuwa na Maboma 126 ya Vyumba vya Madarasa na 58 nyumba za walimu. Serikali katika kuunga mkono juhudi za wananchi mwaka 2005/2006 Wilaya ya Nzega ilipatiwa Ruzuku ya jumla ya shilingi milioni 32.1, zikiwemo shilingi milioni 77.5 ujenzi wa vyumba vya madarasa na shilingi milioni 46.8 za ujenzi wa nyumba za walimu.

Milioni 7.13 za ununuzi wa madawati, shilingi milioni 26.4 kununua vivunge vya Hisabati na shilingi milioni 164.3 Ruzuku ya Uendeshaji. Kwa mwaka 2006/2007 Serikali ilipatia Wilaya hiyo shilingi milioni 211.8 zikiwemo shilingi milioni 80.6 za ujenzi wa madarasa, shilingi milioni 126.0 nyumba za walimu na shilingi milioni 5.2 za kununulia madawati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imetekeleza dhamira ya kupeleka madaraka na fedha kwa wananchi. Kwa hiyo, fedha za MEM zimekasimiwa moja kwa moja katika Bajeti za Halmashauri. Kufuatia utaratibu huu Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepata shilingi milioni 85 kwa ajili ya shughuli za ujenzi.

Hivyo ni wajibu wa Halmashauri kuona namna bora ya kutumia fedha hizo kukamilisha maboma yaliyobaki.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kuwakatisha tamaa wananchi, kwani inautambua mchango wao mkubwa katika kuendeleza elimu. Serikali inajitahidi kuhakikisha kuwa fedha inapopatikana inapelekwa mara moja katika maeneo yanayohusika ili kutekeleza kazi zilizopangwa. (*Makofi*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini ukiangalia jinsi alivyojibu katika jibu lake 2005/2006 Serikali ilitenga shilingi milioni 321, 2006/2007 Serikali ilitenga bilioni 211, 2007/2008 imetenga milioni 85 sasa ukiangalia Serikali inashuka wakati wananchi wanapanda katika kuchangia nguvu zao. Hapo ndipo swali linakuja. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, haoni kwamba kutenga hizo fedha kidogo inadhoofisha kutimiza yale majengo ambayo wananchi wamechangia na yanangoja fedha za Serikali?

Mheshimiwa Spika, lakini inakuja vilevile wananchi hawa hawa wanakuwa wanachangia kwenye majengo ya shule za msingi lakini vilevile wanajenga kwenye majengo ya Shule za sekondari. Kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 Serikali imepunguza kiwango cha fedha za majengo ya sekondari katika mikoa yote bado nauliza hivi kinachotokea ni kitu gani wananchi wanachangia, wako tayari. Kwanini Serikali inakuwa inapunguza pesa zinazokwenda kuunga mkono nguvu za wananchi? Naomba majibu ya uhakika.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana kwa kuwa mwana harakati na aliyeguswa sana katika juhudi hizi za kukuza elimu katika nchi yetu, Hongera sana Mheshimiwa Mbunge.

La pili naomba niseme kwa ujumla fedha ya MEM na MMES zimepungua kwa sababu kiasi cha fedha kilizopatikana zilikuwa ni kidogo na hivyo kila mkoa ulikuwa umepewa fungu na mkoa ndipo unapokaa kutoa kipaumbele kwa kila Halmashauri kutegemea mahitaji na uhalisia wa mambo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri Wizara au Serikali ingependa kuona maboma yote yanafunikwa lakini fedha hatuna. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya kila liwezekanalo kwa kadri fedha zitakapopatikana ili kuhakikisha kwamba maboma yanafunikwa.

Aidha, naomba nitoe wito kwa wananchi wote na Halmashauri zote na watendaji wetu wote kwamba fedha hizo chache zilizopelekwa ni kwa ajili ya kufunika maboma yaliyoanzwa na wananchi na si kwa kuanza ujenzi mpya kwani wakizitumia kuanzia ujenzi mpya tutaongeza idadi ya maboma.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya kuzekua maboma hayo hazitoshelezi tena kununua vifaa kwa sababu ya kupanda kwa bei ya vifaa, je, Serikali iko tayari kuongeza fedha hizo ili zitosheleze kuzekua maboma hayo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Spika, naomba tu niwe muwazi kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, fedha hiyo ndiyo tuliyopata na nitakuwa si mkweli nikisema nitaongeza kwa kufidia kutokana na kupanda kwa gharama. Tunawaomba sana tutumie kiasi hicho kidogo cha fedha kilichopatikana kwa ajili ya kuzekua maboma hayo na katika bajeti inayokuja tutaiandaa tukizingatia mfumko wa bei, ahsante.

Na.110

Upangaji wa Wanafunzi Katika Shule

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI aliuliza:-

Kwa kuwa ziko shule nyingi za *High School* zinazojengwa na wananchi kwa lengo la kujikwamua kielimu na kwa kuwa shule hizo hupangiwa wanafunzi katika sehemu mbalimbali za nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kuwa shule hizo zilizo pembezoni mwa nchi zinapangiwa wanafunzi zaidi kutoka kwenye maeneo yanayozunguka shule kuliko kujaza watoto wa kutoka nje ya maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalysi Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaochaguliwa kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano hupangwa katika makundi matatu kulingana na mpangilio wa masomo yaani (*subject combinations*) ambayo wanafunzi wenyewe huyachagua. Aidha, wanafunzi wakiwemo wanaotoka maeneo ya pembezoni mwa nchi wako huru kuchagua shule ambayo wanapenda wakasome kwa kuzingatia michanganuo yao ya masomo na kwa msingi huo tunajenga Utaifa. Kamati ya Uchaguzi wa kidato cha Tano, huwapanga wanafunzi katika makundi ya masomo kulingana na ufaulu wao katika masomo hayo. Mwanafunzi anayestahili kuingia Kidato cha Tano hupangwa katika shule kwa kuzingatia ufaulu wake, kuwepo kwa masomo na nafasi katika shule hiyo. Kwa hiyo, shule zilizo pembezoni mwa nchi hupangiwa wanafunzi waliochagua kupangwa huko. Ikiwa nafasi katika shule hizo zitakuwa wazi zitajazwa na wanafunzi wa karibu wenye sifa za kuingia Kidato cha Tano ambao pia wamekosa nafasi katika shule walizochagua. Hata hivyo, lengo la sasa ni kila Tarafa kuwa na Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na cha Sita ambazo zitachukua wanafunzi wengi kutoka maeneo jirani kwa kuzingatia ufaulu na masomo wanayochagua.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nitauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa vile mazingira magumu ya elimu katika maeneo ya pembezoni mwa nchi au maeneo ambayo hayajaendelezwa sana hapa nchini wanafunzi katika maeneo hayo wanashindwa kushindana kitaaluma na maeneo ambayo yameendelea au maeneo ya mijini? Je, anakubaliana na mtazamo huo?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa vile maeneo mengi ya vijijini ambayo ni pamoja na maeneo ya Ludewa kwa mfano wananchi ni fukara sana na wanashindwa kuboresha mazingira ya taaluma katika maeneo hayo, je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia

na kuhakikisha kwamba na maeneo hayo kitaaluma yananyanyuka ili kupunguza *gap* ya kitaaluma kati ya maeneo ya vijijini na maeneo ya pembezoni na yale maeneo yaliyoendelea na maeneo yaliyo mijini? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru na yeye pia kwa namna ya kipekee kwa jinsi ambavyo yuko mstari wa mbele kutetea masuala ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu kwamba Serikali inatambua kwamba yako maeneo yaliyo nyuma kielimu na yapo katika mazingira magumu. Kwa kutambua hilo, mwaka jana tulitoa fedha nyingi katika Mikoa ambayo jumla iko Mikoa nane. Mwaka huu tumetoa maelekezo kwamba fedha zilizopelekwa kwa ajili ya *MMEM* pamoja na *MMES* zitoe kipaumbele zaidi kwenye maeneo ambayo miundombinu yake ni hafifu au mazingira ya elimu hayavutii na vyovyote vile kwa sababu moja au nyingine yanasababisha kudorora kwa masuala ya elimu. Uamuzi wa kufanya hivyo uko mikononi mwa uongozi wa Mkoa kwa sababu fedha hizo wamepelekwa wao na kwamba ziende wapi na zikafanye nini, ni jukumu lao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushindwa kwa wanafunzi kushindana kitaaluma na kwamba wanaweza wasi-*perform* vizuri pamoja na wenzao, kwa niaba ya Waziri wa Elimu naomba niseme tumeelekeza Wakaguzi wetu wa Kanda waweze kufanya ukaguzi wa kina kuona pale ambapo pana dosari na ambapo pana mapungufu ili tuweze kupafanyia kazi kitaalam.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Serikali imepanga na imetoa mwelekeo wa kwanza kabisa katika elimu. Tunaahidi kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha elimu inakuwa bora na siyo bora elimu. Huu ni mwanzo, nina hakika tutafika na tutafanikiwa endapo sote kwa pamoja tutashirikiana.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, hili swali linahusu shule za sekondari na kwa sababu kuna jambo muhimu linavuma kwenye vyombo vya habari kwamba mtihani wa *Form Two* ume-*leak*, je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu suala hili na imechukua hatua gani?

SPIKA: Hilo ni swali jipya wala halihusiani na na swali la awali. Tunaendelea Waheshimiwa na Wizara ya Nishati na Madini na swali linaulizwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala.

Na.111

Leseni za Utafiti wa Madini

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi ya Jimbo la Msalala zimetolewa leseni za utafiti wa madini (PL) kwa kampuni kubwa:-

(a) Je, ni kampuni gani zenye leseni za kutafuta madini katika maeneo ya Kalole (Nyangalata), Nyamakwenge, Mwazimba, Misolele, Malito na Masabi?

(b) Je, leseni hizo zilitolewa lini kwa mara ya kwanza kabla ya kuanza kuhuishwa (*renewal*) na zitaisha lini na maeneo gani yameachwa wazi kwa mujibu wa Sheria ya Madini inayomtaka mmiliki wa leseni kuacha sehemu ya eneo analomiliki kila anapohuisha (*renew*) leseni yake?

(c) Kwa kuwa ni nia ya Serikali kuwatafutia maeneo wachimbaji wadogo wadogo, je, ni maeneo gani kati ya hayo niliyotaja yanafaa kijiolojia kwa wachimbaji wadogo pekee?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa maeneo mengi ya Jimbo la Msalala, Wilayani Kahama, yametolewa leseni kubwa za utafutaji wa madini (*prospecting licenses*). Kampuni zenye leseni katika Jimbo la Msalala ni pamoja na kampuni ya Pangea Minerals Limited, yenye leseni katika eneo la Kalole (Nyangalagata), TANZAM 2000 na Northern Mining and Consulting Limited, zenye leseni katika maeneo ya Nyamakwenge, Barrick Exploration Africa Limited, yenye leseni katika eneo la Mwazimba, Pine Wood Resources Limited, yenye leseni katika maeneo ya Malito na Misolele na National Mineral Development Corporation (NMDC) ya India yenye maombi ya leseni ya utafutaji madini katika eneo la Masabi.

(b) Mheshimiwa Spika, leseni zinazomilikiwa na kampuni nilizozitaja katika jibu la sehemu (a) zilitolewa kwa vipindi tofauti na hivyo kumaliza muda wake kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, leseni iliyotolewa kwa Pangea Minerals Limited katika eneo la Kalole (Nyangalagata), ilitolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu kuanzia tarehe 5 Juni, 2006 hadi tarehe 4 Juni, 2007 na kuhuishwa kwa mara ya kwanza hadi tarehe 4 Juni, 2009; leseni ya TANZAM 2000, ilitolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu katika eneo la Nyamakwenge kuanzia tarehe 23 Februari, 2004 hadi tarehe 22 Februari, 2007 na kuhuishwa hadi tarehe 22 Februari, 2009; leseni ya Northern Mining and Consulting Company Limited ilitolewa kipindi cha awali cha miaka mitatu katika eneo la Nyamakwenge tarehe 15 Agosti, 2001 hadi tarehe 14 Agosti, 2004 na itamaliza muda wake tarehe 14 Agosti, 2008 baada ya kuhuishwa kwa vipindi viwili vya miaka miwili miwili; leseni ya Barrick Exploration Africa Limited ilitolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu katika eneo la Mwazimba tarehe 30 Aprili, 2005 na itamaliza muda wake

tarehe 29 Aprili, 2008; leseni iliyotolewa kwa Julius S. Matutu katika eneo la Masabi tarehe 28 Juni, 2004 ilikwisha muda wake tarehe 27 Juni, 2007 na sasa eneo hilo limeombwa na kampuni ya *NMDC* ya India; leseni ya kampuni ya *Pine Wood Resources Limited* ilitolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu katika eneo la Malito na Misolele tarehe 10 Februari, 2005 na itamaliza muda wake tarehe 9 Februari, 2008.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyoachwa wakati kampuni hizo zilipohuisha leseni zao na kuachia eneo la leseni yake kwa mujibu wa Sheria ya Madini yamekuwa yakiombwa na waombaji wengine.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeanzisha utaratibu wa kuainisha maeneo yanayoweza kufaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kuangalia uwezekano wa kuyatenga kuwa maalum kwa ajili ya wachimbaji hao kwa mujibu wa sheria. Lengo la zoezi hilo ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata maeneo ya kuendesha shughuli za uchimbaji madini kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia matokeo ya utafiti unaofanywa na kampuni zenye leseni za utafutaji madini katika maeneo mbalimbali ili kupata maeneo yatakatayofaa kutengwa kwa wachimbaji wadogo pekee na mengine kubakia kwa uchimbaji mkubwa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake hasa vipengele (a) na (b) vya swali langu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa maeneo hayo niliyoyataja ni maeneo ambayo ni makazi ya watu na kuna watu zaidi ya 50,000 ambao wamekuwa wakijishughulisha na shughuli za uchimbaji katika maeneo hayo, je, Serikali kwa nini isifanye uamuzi wake yenyewe wa kusema kwamba leseni fulani itakapoisha haitahuishwa tena ili eneo hilo libaki kwa wachimbaji wadogo kuliko kuendelea kuhuisha tu wakibadilisha majina ya kampuni na itaendelea hivyo milele kwa sababu maeneo wanayapenda?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Serikali inafahamu kwamba kampuni inayofanya utafiti kwa jina la utafiti katika eneo la Mwazimba, *actual* haifanyi utafiti inachimba kwa sababu kila baada ya siku mbili, tatu Wazungu wale wamekuwa wakisafirisha dhahabu kutoka eneo la Mwazimba kwenda Mwanza? Sijui Serikali inafahamu jambo hilo kwamba wanachokifanya ni kuchimba na siyo utafiti na wana udhibiti gani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na mkanganyiko wa uelewa wa leseni hizi ambazo hutolewa. Wale wote wanaopewa leseni za utafutaji, hawaruhusiwi kwa mujibu wa sheria kufanya uchimbaji na utafiti wa madini hauchukui eneo kubwa kiasi kwamba watu wanalazimika kuhamishwa. Wakati mwingine, huwa tunatoa mifano hata Mji huu wa Dodoma unaweza kuwa chini ya leseni ya utafutaji. Mtafutaji anapopata eneo tu ambalo anataka kuchimba

pale kwa sababu ya utafiti wake ndio wataelewana na yule pale ambapo anataka kuchimba. Iwapo atabaini madini au mafuta hapa Dodoma, hapo ndio ataanza mchakato kama anaweza kutufidia, akatuhamisha sote hapa Dodoma ili kusudi aendelee na uchimbaji, sawa, lakini kabla ya kupata leseni ya uchimbaji utafiti haujumuishi kumwamisha mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, swali hili nimejibu nikioanisha na swali la pili la utafiti wa Mwazimba ambapo inasemekana kuna mtafiti lakini anaendelea kuchimba. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge ana taarifa hizo anaweza akazitoa vile vile kwa Maofisa wetu wa Kanda ambao ni kazi yao kupitia kila wakati kuhakikisha kwamba kama huyu kweli anachimba madini kwa sababu ya biashara tutamchukulia hatua na kumfutia leseni mara moja. Wakati mwingine huwa anachukua zile *samples* katika maeneo mbalimbali ambazo na zenyewe huwa zinahakikiwa na Maofisa wetu wa madini ndio hapo watu huwa wanafikiria kwamba zile *samples* anazozifanyia utafiti ni madini ambayo yanachimbwa na kutoroshwa. Lakini ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa kuwatetea wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo anapoishi na mimi nimefika pale nikaona juhudi zake, ninampongeza na aendelee hivyo hivyo.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Nikisikia suala la madini, ninashindwa kukaa, naona kiti hakikaliki kwa sababu ya mambo ambayo ni kama hayo yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba kuna mkanganyiko mwingi sana wa kuelewa hizi sheria, je, Wizara yake au Serikali kwa ujumla inachukua hatua gani ili kuweza kufafanua mambo hayo kwetu sisi viongozi na hata kwa wananchi na wale wadau husika? Ni utaratibu gani ambao wamechukua na hasa ukizingatia sheria tumeisubiri muda mrefu, sheria italetwa lini? Inatakiwa uwe kwenye eneo uelewe tatizo ni nini.

Mheshimiwa Spika, ninavyoongea hapa kuna ujumbe wa watu 18 wako hapa wanakusudia kumwona Waziri kwa ajili ya matatizo ya madini, mpaka lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ambaye kila wakati amekuwa anakuja pale ofisini kwetu kuhakikisha kwamba tatizo ambalo lipo katika Jimbo lake linatatuliwa hususani la wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ameeleza kweli nilivyosema kwamba kuna uelewa mdogo wa sheria, tumekuwa tunakutana anaielewa. Sasa hivi ukisoma kwenye kitabu changu cha bajeti tumesema kwamba tutaruhusu Sera za Madini ambayo ni ya mwaka 1997 ambayo itaelekea kuboresha Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Lakini kabla ya kufanya hivyo, Wizara yangu itaandaa semina maalum ambayo itapelekwa kwa wadau lakini vile vile tutajitayarisha kufanya semina kwa Bunge zima ili sote kwa pamoja twende pamoja katika uelewa wa hizi sheria ambazo zinaongoza sekta ya madini.

MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa swali hili linafanana na watu wote wanaokaa katika maeneo makubwa ya Jimbo la Bukene ambao hawajui haki zao pale mwekezaji anapokuja, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha ili na wenyewe wapate leseni au wafanye *joint venture* na hao watu wanapokuja kupata leseni za madini? Kwa mfano pale Itanana kuna almasi na dhahabu na kule Mahene kuna dhahabu, sasa wanapokuja pale wale wananchi ambao wamezaliwa hapo ni sehemu zao za kila siku, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hao wananchi wafanye *joint venture* na makampuni yanayokuja ili waweze kunufaika na kuondokana na umaskini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakubaliana na yeye kwamba wachimbaji wadogo wadogo au watu wenye maeneo ambao ni Watanzania inabidi kupewa mafunzo mbalimbali juu ya sheria zetu na tumekuwa tukifanya hivyo. Tulikuwa tunafanya kwa wachimbaji wadogo lakini tulikuwa hatufanyi kwa watu wenye leseni na watu wenye leseni wenyewe inabidi kujua mambo ya kibiashara, kuna wengine wanachukua leseni hizi halafu baadaye wanaziuza kwa bei ndogo tu kwa wawekezaji wakubwa halafu baadaye wanakuja kulalamika.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba unapokuwa na leseni hakuna mtu yeyote anayekulazimisha ile leseni yako kuitoa kwa mtu, ni wewe tu ukishapata ile leseni iwe ya *prospecting*, ya utafutaji au iwe ya uchimbaji, ni wewe mwenyewe ukitaka kuingia ubia au ukitaka kumuuzia mwingine, inabidi uje mwenyewe utoe uthibitisho wako huo katika Wizara yetu lakini Wizara kama Serikali haikulazimishi. Lakini kwa sababu tumeshaliona tatizo hili, kabla hatujabadilisha leseni ya mzalendo kuiuza kwa mtu yeyote kutoka nje, tutakuwa tunakaa naye tunampa nasaha za kwa nini aiuze, kwa nini asiingie *joint venture*? Nitakubaliana naye na tutaiweka katika mipango yetu ya baadaye, ahsante sana.

Na.112

Ujenzi wa Majosho – Kongwa na Mpwapwa

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa, ni nia ya Serikali kuendeleza na kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo kama majosho, malambo na kadhalika.

Je, kwa mwaka 2006/2007, ni majosho mangapi na malambo mangapi yaliyo maeneo gani yamejengwa katika Wilaya za Kongwa na Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job J. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni nia ya Serikali kuona kwamba miundombinu ya mifugo imefanya kazi ipasavyo.

Serikali inafanya hivyo kwa kiasi kikubwa kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kwa kushirikiana na wananchi na sekta binafsi. Kuanzia mwaka 2003/2004, Serikali ilibuni mipango ya maendeleo ya kilimo Wilayani (*DADPs*), ambapo Wilaya huibua miradi mbalimbali kwa njia shirikishi ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo kama vile majosho na malambo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007, Wilaya ya Mpwapwa ilikarabati joshu la Mbuga kwa jumla ya shilingi milioni 5 na lambo la Iyenge kwa jumla ya shilingi milioni 10. Wilaya ya Kongwa kwa upande wake haikuwasilisha maombi ya ujenzi au ukarabati wa majosho na malambo kwa mwaka 2006/2007 kwa kuwa ilikuwa na vipaumbele vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/2008, Wilaya za Kongwa na Mpwapwa zimewasilisha maombi ya kukarabati miundombinu ya mifugo kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Kongwa itajenga joshu jipya moja la Chitego kwa gharama ya Sh.12,000,000/= na kukarabati majosho sita ya Hogolo Sh.3,500,000/=, Nagesemi (Sh.2,500,000/=), Kongwa (Sh.2,500,000/=), Laikali (Sh.2,500,000/=), Pandambili (Sh.4,500,000/=) na Mseta - Bondeni (Sh.2,500,000/=). Wilaya ya Mpwapwa itajenga majosho manne ya Msagali, Kimagai, Kikuyu na Lufu kwa gharama ya Sh.49,500,000/= na pia itakarabati majosho matatu ya Mwanawota, Winza na Kisima kwa gharama ya Sh.19,500,000/=. Aidha, Wilaya ya Mpwapwa pia imetenga Sh.85,500,000/= kwa ajili ya malambo ya Sazima, Mzase, Kibakwe na Lukole.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wananchi wa Wilaya za Kongwa na Mpwapwa kupitia Waheshimiwa Wabunge wao kwa kuibua miradi ya kujenga na kukarabati miundombinu hii ya mifugo kwa lengo la kuboresha sekta ya mifugo na naomba waendelee na jitihada hizo.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na pia ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Nina maswali mawili madogo ya ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa linahusiana na mwaka 2006/2007 kuwa je, ni majosho mangapi na malambo mangapi yamejengwa katika Wilaya ya Kongwa na Mpwapwa? Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwa ukweli kuwa kwa mwaka 2006/2007, Wilaya ya Kongwa haikuwasilisha maombi ya ujenzi au ukarabati wa majosho na malambo. Sasa hii inaonyesha kwamba ziko Wilaya nyingine ambazo haziona umuhimu wa kuweka vipaumbele katika masuala haya ya malambo na majosho Wilaya mojawapo ikiwa ni Kongwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wake watakuwa tayari kuja Kongwa ili kusaidia kuelimisha uwekaji wa vipaumbele kwa upande wa Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, la pili dogo, Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenyewe na wataalam wao watakubali kufika Kongwa ili kuona eneo la vijiji vya Matongoro na Norini ambapo wananchi wamekuwa wakisema kwamba kuna eneo zuri sana la kuweka bwawa ambalo litasaidia kwa ajili ya mifugo na kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, Wizara iko tayari kwenda Kongwa ili kusaidiana na Mheshimiwa Job Ndugai na wananchi wake kubaini vipaumbele katika sekta ya mifugo hususan katika ujenzi wa miundombinu kama malambo na majosho hasa ukizingatia kuwa Wilaya ya Kongwa ina majosho tisa tu yanayofanya kazi, matano hayafanyi kazi na ina upungufu wa jumla ya majosho matano ili kuhakikisha kuwa mifugo yote waliyonayo wanaweza wakaiogesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa bwawa, Wizara itakuwa tayari kupeleka wataalam wake ili kubaini ustahili wa ujenzi wa bwawa kwa ajili ya maji ya mifugo kwenye maeneo aliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai, kwa jinsi anavyoshughulikia wananchi wake katika harakati za maendeleo hususan maendeleo ya mifugo ambayo ni sekta muhimu sana kwa Wilaya na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla.

Na.113

Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya *MSD*

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza:-

Kwa kuwa *MSD* ndiyo yenye dhamana ya kusambaza dawa na vifaa mbalimbali vya matibabu kwenye Wizara, Mikoa na kwenye Halmashauri za Wilaya, lakini *MSD* inashindwa kufanya hivyo kwenye maeneo husika kutokana na kukosekana kwa baadhi ya dawa:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa mchanganuo wa kiasi gani cha fedha kilitengwa kwa Wizara, Mikoa na kiasi gani kilitumika na kiasi gani kilibaki katika mwaka 2006/2007?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kutenga asilimia 70 ya fedha kwa ajili ya dawa zipelekwe *MSD* na asilimia 30 ipelekwe kwenye Halmashauri za Wilaya, Mikoa na Wizara ili hapo *MSD* inapokosa dawa/vifaa waweze kununua kwa wauzaji wengine walioruhusiwa na Serikali kwa kutumia fedha hizo?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya bei za vifaa kama vile vitanda vya kujifungulia akina mama wajawazito kutofautiana kati ya Mkoa na Mkoa na kati ya Halmashauri za Wilaya mbalimbali?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye vipengele a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitenga Sh.31,803,329,921/= kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba muhimu kwa matumizi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya, Mikoa, Rufaa na Hospitali Maalum za Umma. Fedha hizo zilipelekwa *MSD* na kuwekwa kwenye akaunti ya vituo hivyo ili kuviwezesha kuagiza dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji yake.

Aidha, kiasi kilichokuwa kimebakia hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2007 ni Sh.15,686,816,527/=. Kiasi hiki cha fedha kilichobakia ni kikubwa kwa sababu fedha za bajeti huanza kutolewa miezi miwili au mitatu baada ya kupitishwa na Bunge. Hata hivyo, fedha zilizoingizwa kwenye akaunti ya hospitali, hata kama zitakuwa hazijatumika zote hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, hazirudishwi kwenye Mfuko wa Serikali bali zinaendelea kutumika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, ili kuokoa muda, nitampatia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote nakala ya mchanganuo wa fedha hizo kwa Wizara, Mikoa, Hospitali Maalum, Rufaa na Wilaya.

(b) Kutokana na ugumu wa upatikanaji wa dawa kutoka *MSD* kwa baadhi ya vituo vya kutolea huduma, Wizara yangu inakusudia kuanza kupeleka kiasi cha fedha kwenye Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Hospitali Maalum na za Rufaa ili kuziwezesha kupata dawa na vifaa tiba kutoka kwa wauzaji wengine watakaokubaliwa na Serikali. Utaratibu huu unatarajiwa kuanza mara baada ya hali ya utunzaji wa kumbukumbu za dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma itakapokuwa imeboreshwa.

(c) Bei ya vitanda kwa ajili ya kujifungulia akina mama inayotozwa na *MSD* ni moja kwa nchi nzima. Tofauti ya bei ya vitanda hivyo kati ya Mikoa na Mikoa na kati ya Halmashauri za Wilaya mbalimbali inaweza kuwepo kwa wafanyabiashara binafsi kutokana na uhuru wa soko.

SPIKA: Mheshimiwa Mgana I. Msindai swali la nyongeza!

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa baada ya kufanya utafiti wa zaidi ya Halmashauri 60, inaonyesha kuna mgogoro mkubwa wa upatikanaji wa dawa na hata Maafisa Masuhuli wengi hawajui fedha wanazopewa na fedha zinazobaki, je, Serikali itakuwa tayari sasa kufanya uhakiki upya ili kujua ni fedha ngapi zimetolewa kwa miaka miwili iliyopita na kuwajulisha Maafisa Masuhuli?

(b) Kwa kuwa katika swali langu mimi nilipendekeza 30% ya fedha hizi ziende moja kwa moja kwenye Halmashauri ili wasiendelee kupata taabu ya kununua dawa wakati wanapokuta dawa hazipo, je, Serikali inakubaliana na mimi katika pendekezo hili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Halmashauri 60 zina migogoro na hawajui kiasi cha fedha walichopatiwa, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba si kweli kwa sababu hawa Maafisa huwa wanapelekewa migawo yao ya pesa ambazo ziko kule *MSD*. Lakini hata hivyo tutafuatilia kwa karibu zaidi ili kuona wale ambao hawajapata taarifa hii ili tuweze kuwapatia.

Lakini vilevile naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sisi kama Wizara tutatoa nakala vilevile kwa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuwaonyesha ni pesa kiasi gani *MSD* imetenga katika kila Wilaya ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia na kuweza kuangalia katika Halmashauri zao kuona kwamba orodha tuliyowapa inarandana na ile ambayo imepelekwa katika Halmashauri zao?

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mgana I. Msindai kwamba 30% ya fedha zile tuzipeleke katika Halmashauri lakini kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali tumeshaona kwamba kuna umuhimu wa kupeleka kule. Tunapokea ushauri wake na tutaufanyia kazi ili kuweza kuona ni kiasi gani tutakubaliana, Serikali pamoja na Wabunge mtapata taarifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mwongozo wa Spika!

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 55(3) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 114 inayohusu wageni na Kanuni ndogo 3(a) inayohusu mavazi.

Mheshimiwa Spika, kuna tukio ambalo lilitokea ambalo nilitaka nikuombe ulitolee ufafanuzi. Juzi tarehe 5/11/2007 kuna Kiongozi mmoja wa Chama cha Mapinduzi, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mbeya, alikuwa aje anione hapa Bungeni na tulikubaliana aje saa 3.30 asubuhi kwa sababu tunalima chai wote kule Lushoto. Sasa alipofika kwenye mlango wa kuingilia ukumbini alikuwa amevaa sare ya Chama cha Mapinduzi, Askari Polisi mmoja alimwambia kwamba haruhusiwi kuingia kwenye eneo la Bunge na sare ile. Nikatoka mimi sikumkuta akawa ameondoka lakini jana akaja na nikaenda nikamchukua tukaenda kwenye ofisi hapo nikazungumza naye nikamaliza

akanieleza masikitiko yake kwamba kama Bunge linazuia wananchi kuingia mahali hapa kwa sababu ambazo hazieleweki anashangaa. Nikamwambia hapana! Kanuni zetu zipo wazi kabisa, kuna masharti ya mavazi ya Wabunge wakiwa ndani ya ukumbi, halafu kuna masharti ya wageni wanaoingia kwenye ukumbi na katika hii Kanuni ndogo niliyoisema inaeleza yafuatayo:-

“Pamoja na mengine yote bila kuathiri masharti ya jumla ya fasili ya pili inayohusu wageni, wageni inawabidi wavae mavazi ya heshima kabla ya kuingia katika ukumbi wa mikutano ya Bunge”

Mheshimiwa Spika, sasa ningepomba hili ulitolee ufafanuzi ili kiongozi yule kwa kweli na viongozi wengine waelewe kwamba hatuna Kanuni inayomzuia mtu yeyote kuvaa nguo yake akija kwenye Bunge isipokuwa anapoingia kwenye ukumbi huu anatakiwa avae nguo nadhifu na za heshima na ile sare, haikatazwi mtu kuingia kwenye ukumbi wa Bunge na sare ya chama chake, huko nje na siyo huku ndani na hata humu ndani sidhani kama tumepewa Kanuni hiyo. Kwa hiyo, ungelitolea ufafanuzi ili tuelewane vizuri na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa William H. Shellukindo na ufafanuzi ni kama ifuatavyo:-

Kuna tofauti kati ya ndani ya Ukumbi wa Bunge na nje ya Ukumbi wa Bunge lakini katika maeneo ya Bunge. Sasa mwananchi anayevaa sare za chama chake anaruhusiwa kuingia kwenye maeneo ya Bunge lakini si ndani ya ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo, kama alizuiliwa kwenye geti si sahihi, ilitakiwa angefika hapa sasa kujaribu kuingia ndani ya ukumbi huu hapo angezuiwa na siyo chama kimoja bali ni vyama vyote na hili pia linawahusu Waheshimiwa Wabunge hatumtazamii Mbunge aingie humu ndani na nguo ambayo ni dhahiri kabisa inaashiria kwamba amekuja humu akiwa amejazwa itikadi ya chama chake kwa sababu hatupendi hapa kutokea jambo ambalo linaweza kutafsiriwa na wengine kwamba linaweza kusababisha fujo. Kwa hiyo, ni marufuku ndani ya ukumbi huu kuja na sare uwe ni Mbunge au si Mbunge lakini kwa nje ya ukumbi huu ni ruksa na kukaa na mwananchi pale kantini ukiwa na sare ya *CHADEMA*, *NCCR* au ya *TLP* au *CUF* ni halali kabisa kwa sababu ndivyo walivyo wananchi wetu lakini ndani ya ukumbi ndipo inakataliwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naanza na wageni, naomba nitakapowataja wageni mmoja mmoja basi waweze kusimama ili Waheshimiwa Wabunge wawatambue.

Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Chikawe, anao wageni wake ambao ni kaka yake Padre Hiu Chikawe, ambaye anaishi Tamper Florida, yule pale karibu sana Padre. Tumezoea kuona Wamisionari wanatoka Ulaya na Marekani kuja huku lakini wewe ni Mmissionari umetoka Tanzania kwenda kuhubiri Marekani, hongera sana. (*Makofi*)

Tunaye *Sister Ledocosta Theresia Mhagama wa Chipole Benedict Sisters*, Songea Ruvuma, karibu sana *sister*. Pia miongoni mwao yupo ndugu Diana Kardash wa *Indian Shows Florida* yule pale, karibu sana na mwisho yupo Padre Angelo Msele wa *Benedicts Mission* ya Hanga, Songea, karibuni sana. Tunashukuru mmekuja kujionea wenyewe shughuli za Bunge letu hapa na nawahakikishia tu ndugu yenu Mheshimiwa Chikawe anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Vikao vya Kamati, Mheshimiwa William Shelukindo, ameniomba nitangaze kwamba leo saa tano asubuhi, Kamati Ndogo ya Uwekezaji na Biashara itafanya mkutano wake ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje kwamba kutakuwa na kikao leo saa saba mchana, ukumbi namba 219. Natumaini wale wa Uwekezaji na Biashara watakuwa wamemaliza kwa sababu hawa wao wanaanza saa tano, ni ukumbi uleule.

Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga, Mwenyekiti Kamati ya Miundombinu, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwamba kutakuwa na kikao leo saa nne na nusu yaani sasa mara tutakapositisha hapa, katika ukumbi namba 428, ghorofa ya nne.

Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, ameniomba nitangaze kwamba saa tano kamili katika ukumbi namba 231, anaomba Wajumbe wote wa *PAC* wakutane hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna maonyesho katika sehemu yetu ya tafrija yanayohusu matumizi ya mafuta ya *petrol, diesel* na hifadhi ya mazingira kwa njia ya mafuta yaitwayo *Fuel Reformulator*. Faida ya mafuta hayo ni kupunguza matumizi ya mafuta, kupunguza moshi kwenye magari, kuongeza nguvu ya gari na kuongeza uhai wa *engine*. Wataalamu watakuwa pale kuwawasaidia Waheshimiwa Wabunge kuhusu upatikanaji wa mafuta haya na faida zake.

Kwa hiyo, wakati wowote ambapo mtajisikia huru basi wenye maonyesho hayo watakuwepo kuwaonyesha hayo mafuta ya *petrol*. Tangazo hili linamhusisha Mheshimiwa Kate Kamba, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, yeye anahusika sana na maonyesho haya. Kwa hiyo, atakuwepo kwenye viwanja vya tafrija wakati wowote tutakavyoondoka humu ndani.

Naomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, tukutane kesho mara baada ya Swala ya Ijumaa, mnamo saa nane na nusu. Mkutano huu ni muhimu kwa ajili ya kuendelea kupanga shughuli zetu za Bunge.

Kwa wale Wabunge waliokuwepo kati ya mwaka wa 1970-75, nadhani ni Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya peke yake, Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Stephen M. Wasira, mwenzetu Rev. Kanali Nangugu amefariki dunia kule Tandahimba. Taarifa hizi zimeletwa na Mheshimiwa Juma Abdalah Njwayo. Kwa hiyo, wale walio karibu na marehemu, wanaombwa wamwone Mheshimiwa Njwayo kuelewa mipango ilivyo ya mazishi na kuweza kusaidia kwa njia yeyote ili kumsitiri mwenzetu.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea malalamiko kwamba katika geti kuu la kuingilia katika maeneo ya Bunge kumeanza kutokea usumbufu usio wa kawaida. Suala hili nadhani itabidi nilifanyie kikao na wahusika hivi leo na tutatoa maelekezo ambayo yanazingatia kulinda usalama lakini hayafikii kiwango pia cha uzalilishwaji Waheshimiwa Wabunge. Ni lazima tuweke mezania sawa isiwe tena usalama humo humo baadhi ya vijana wanachukua fursa sasa maana Wabunge nao si kwamba wanapendwa na kila mtu. Mambo mengine ambayo yameelezwa katika vikaratasi hapa nadhani yamezidi na yamekiuka kabisa lengo la usalama. Kwa hiyo, kesho tutawatangazieni utaratibu mpya na mzuri juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mwenyekiti wa Wabunge wanaotoka katika Mikoa inayolima Korosho anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wadau wa zao la Korosho, mkutane hapo nje, mara baada ya kusitisha shughuli kwa asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwenye orodha ya shughuli za leo, tunao Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi. Taarifa niliyoipata kwa Mheshimiwa Mohamed H. Missanga ni kwamba Muswada huu utakuwa tayari kwenye kipindi cha jioni, bado wana majadiliano na Wizara husika na limethibitishwa hilo na Waziri wa Miundombinu. Sasa kutokana na hilo, nichukulie kuorodheshwa kwa shughuli ya Muswada huo inahusu kikao kitakachoendelea jioni. Kwa maana hiyo basi, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

(Saa 4.50 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 *(The National Construction Council (Amendment) Bill, 2007)*

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru tena kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuwasilisha hoja mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi (*The National Construction Council (Amendment) Bill, 2007*) pamoja na marekebisho yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi (*The National Construction Council Act, 2007*). Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi, niseme ilitungwa mwaka 1979. Lengo lilikuwa ni kuunda chombo cha kuchochea maendeleo katika sekta ya ujenzi nchini kwa njia ya kupanga mipango, kuratibu, kutoa ushauri na mafunzo, kufanya utafiti, kusambaza taarifa, kuandaa majarida mbalimbali ya kiufundi na utatuzi wa migogoro katika sekta ya ujenzi. Sheria hii imeonekana kwa sasa kuwa ina mapungufu mengi na hivyo kutokidhi mahitaji ya sekta kufuatana na mabadiliko mbalimbali katika sekta yenyewe ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuifanyia marekebisho Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi ili kuliimarisha Baraza hilo na kuliwezesha kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza, inahusu masharti ya utangulizi ambayo ni jina la sheria na uhusiano wake na Sheria Mama ya Mwaka 1979 ambayo ndiyo inapendekezwa ifanyiwe marekebisho. Sehemu ya pili ni marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha pili, tatu, nne, tano, sita, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na sita na kumi na tisa pamoja na jedwali lililopo katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili ya Muswada, pendekezo la kwanza ni kuongeza tafsiri mpya kama zinavyoonyeshwa katika ukurasa wa 50 wa Muswada ambapo kifungu cha (2) cha Sheria Mama kinarekebishwa na kubadilisha cheo cha Katibu Mtendaji anayeongoza Baraza hilo kuwa Mtendaji Mkuu (*Chief Executive Officer*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika ukurasa wa 50 mpaka 52 wa Muswada ambapo kifungu cha (4) cha Sheria kinarekebishwa kwa kuboresha majukumu ya Baraza ili kulipa nguvu za kisheria Baraza hilo na uwezo wa kufanya kazi kwa ubora na ufanisi. Majukumu ya Baraza yanayopendekezwa ni kumi na tano badala ya kumi na tatu yalivyo hivi sasa. Katika majukumu hayo kumi na tano yafuatayo yametokana na kuhuishwa kwa majukumu ya zamani ili kutoa mwelekeo na uwazi. Kubwa ni kukuza maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini, kutoa ushauri kwa wadau wa sekta ya ujenzi, upashanaji habari, usimamizi wa viwango, kukuza teknolojia ya ujenzi nchini na kuandaa mikutano. Aidha, majukumu mapya yanayopendekezwa yanahusisha majukumu muhimu yafuatayo:-

- Kufanya tathmini ya maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini, kukuza ubora wake pamoja na kufanya ukaguzi wa kiufundi.

- Kutekeleza na kusimamia kanuni za mazingira na afya katika kanuni za ujenzi.

- Kukuza biashara ya nje kwa huduma za ujenzi na utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu liko katika ukurasa wa 52 wa Muswada ambapo kifungu cha (5) cha Sheria kinarekebishwa kwa kuwezesha Baraza kuwa mratibu yaani *focal point* wa taasisi zote zinahusika na shughuli za ujenzi katika sekta za ujenzi na kuondoa neno kuwa kiongozi kama ilivyopendekezwa awali katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la nne liko katika ukurasa wa 52 ambapo kifungu cha (6) cha Sheria kinarekebishwa. Marekebisho hayo yanalenga katika kubadili kama nilivyoeleza cheo cha Katibu Mtendaji kuwa Mtendaji Mkuu (*Chief Executive Officer*). Aidha, Mtendaji Mkuu wa Baraza hilo sasa atakuwa anateuliwa na Waziri mwenye dhamana wa masuala ya ujenzi badala ya kuteuliwa na Rais kama ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tano liko katika ukurasa wa 53 wa Muswada ambapo kifungu cha (9) chote kinafutwa kwani suala zima la kuundwa Kamati lipo katika kifungu cha Kumi cha Sheria, hivyo hakuna haja ya kulirudia rudia. Kamati hizo zitaundwa pale itakapoonekana ipo haja ya kufanya hivyo kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa malengo ya msingi wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la sita katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika ukurasa wa 53 ambapo kifungu cha 11 cha Sheria kinarekebishwa kwa kumtaka mtu yeyote atakayejihusisha na shughuli za ujenzi au atakayejihusisha na shughuli za usajili katika taaluma ya ujenzi kutoa taarifa kama Baraza litakavyomtaka kutoa taarifa husika. Aidha, inapendekezwa kuwa mtu atakayeshindwa au kukaidi kuwasilisha taarifa husika kwa Baraza hilo na atapatikana na hatia basi apigwe faini ya Sh.500,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la saba katika sehemu hii lipo katika ukurasa wa 53 ambapo kifungu cha 16 cha Sheria kinarekebishwa kwa kulitaka Baraza kuweka na kutunza vitabu vya akaunti na kumbukumbu nyingine. Vitabu vya fedha vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kulingana na Sheria ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la nane katika eneo hili lipo katika ukurasa wa 53 hadi ukurasa wa 54 wa Muswada ambapo kifungu cha 19 cha sheria kimeongezwa ili kumpa mamlaka ya kisheria Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni za kurahisisha utekelezaji wa sheria kuhusu malengo na majukumu ya Baraza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tisa katika eneo hili lipo katika ukurasa wa 54 mpaka 55 wa Muswada ambapo jedwali la Sheria linarekebishwa kwa kuongeza sifa za Mwenyekiti wa Baraza hilo atakayeteuliwa na Rais kuwa awe na uelewa wa kutosha na uzoefu wa kutosha wa masuala ya sekta ya ujenzi. Aidha, sehemu hii pia inapendekeza idadi ya wawakilishi wa wajumbe wa Baraza kuwa kumi na nne ambapo wajumbe saba watatoka sekta ya umma na wajumbe wengine saba watatokana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, niruhusu nichukue nafasi hii, nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni yao Jijini Dar es Salaam tarehe 24 Oktoba, wakati wa kikao cha wadau yaani *public hearing*. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha Muswada huu, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoutambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini kwa ushirikiano wa karibu walionipa wakati wa kikao hicho na pia wakati wa kuchambua Muswada huu kifungu kwa kifungu. Tunaishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge. Uchambuzi wao wa kina wa Muswada huu walioufanya ndiyo umewezesha Muswada huu kuwasilishwa jioni hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunaishukuru Kamati kwa dhati kwa kutuunga mkono katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu pamoja na orodha ya marekebisho iliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru pia Manaibu Waziri wa Wizara yangu Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari pamoja na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu Dr. Enos Bukuku na Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Omar Chambo pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima ya kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria wa Baraza la Taifa la Ujenzi (*The National Construction Council (Amendment) Act, 2007*). Sasa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kisha liupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. FELIX N. KIJIKO (K.n.y. MHE. MOHAMMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nami niwapongeze wale wote walioshinda katika uchaguzi

kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi Mkuu wa CCM ulioisha hivi karibuni ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa upande wa Tanzania Visiwani, Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa, Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa na Mheshimiwa Yusuph Ally Makamba, Katibu Mkuu wa CCM Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba niwapongeze Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao ni Mheshimiwa Andrew John Chenge, Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Mawaziri wa Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa ushindi wao wa kishindo wa kuchaguliwa kwao kuwa Wajumbe wa *NEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Tisa wa Bunge, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Marekebisha ya Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi, Sura ya 162 ili kutoa mapendekezo yatakayoboresha sheria hiyo na kuifanya itekelezeke kwa ufanisi. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Miundombinu pamoja na Watendaji wa Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Maoni ya Kamati ya yangu ya Miundombinu, napenda kuweka kumbukumbu sawa katika *Hansard* ya tarehe 6 Novemba, 2007, kwamba, kuchelewa kuwasilishwa kwa Muswada huu Bungeni kama ilivyokuwa imejitokeza katika *Order Paper* ya tarehe 6 na 7 Novemba, 2007 ni kutokana na maombi ya Serikali na wadau ili kupata muda wa kujadiliana kuhusu baadhi ya vifungu vilivyokuwa na utata. Kwa maoni ya wadau, baadhi ya vifungu vilikuwa vinapingana na baadhi ya sheria zilizoanzisha Bodi za Kitaalam zilizo chini ya Wizara ya Miundombinu. Kwa bahati mbaya, majadiliano yalichukua muda mrefu kuliko ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wetu, Kamati ilikwishakamilisha taarifa yake isipokuwa tulikuwa tukisubiri muafaka kati ya Serikali na wadau. Napenda kukutaarifu kuwa maafikiano hayo yaliridhiwa na pande zote mbili ambayo pia Kamati imeyaridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 69(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau husika wa Muswada wa Sheria hii ya Baraza la Taifa la Ujenzi na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 24 na 25 Oktoba, 2007 katika vikao vilivyofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru na kuwapongeza kwa dhiti wadau wote muhimu kwa ushiriki wao katika kuandaa Muswada huu. Wadau hao ni kutoka sekta na taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali kama vile Baraza la Taifa la Ujenzi, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu, Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala wa Majengo na Wakala wa Ufundi na Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mamlaka ya Udhibiti wa Zabuni, Chama cha Washauri, *K & Associates Ltd, Crown Agents, Lomo Consult, Howard Humphreys* na wengine wengi ambao kwa pamoja walitoa michango mizuri kwa ajili ya kuboresha Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachilia mbali Wizara husika ya Miundombinu, Kamati ilishirikisha pia Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara ya Fedha katika kupata ufafanuzi na maoni zaidi juu ya namna ya kuboresha sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Muswada huu yanalenga kuboresha Sheria iliyopo ya Baraza la Taifa la Ujenzi; ikiwa ni pamoja na kuifanya itekelezeke. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya marekebisho haya kwani kuwepo kwa sheria isiyotekelezeka ni kikwazo katika kufikia malengo yaliyokusudiwa na hivyo kurudisha nyuma jitihada za kuleta mabadiliko chanya katika fani ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ya sheria hii ambayo yatawezesha Baraza kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri sahihi na kwa wakati kwa Serikali na wadau wengine wa sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza kama chombo cha kuchochea maendeleo ya ujenzi nchini, liendeleo kutoa kipaumbele katika kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu masuala ya ujenzi. Hii itaongeza ufanisi wa kazi zao na kuboresha sekta hiyo. Vilevile Kamati inasisitiza kuwa Baraza hili liendeleo kuandaa na kutoa mafunzo mbalimbali kwa wadau wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa malengo ya Muswada huu ni mazuri kwa manufaa na maslahi ya maendeleo ya Taifa letu, Kamati inashauri Serikali itoe kipaumbele katika kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya ujenzi. Kuwepo kwa Sera na Sheria nzuri katika sekta ya ujenzi hakutakuwa na maana yoyote iwapo hakutakuwa na fedha za kukamilishia malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inalipa Baraza pamoja na mambo mengine, jukumu la kupanga mipango ya kitaalamu ya kiujenzi. Kamati inaishauri Serikali

kuzingatia ushauri unaotolewa na Baraza hili na wadau wake katika kutekeleza mipango ya kimaendeleo. Serikali iendelee kuwatumia wataalamu wazalendo na kuthamini taaluma na ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa taarifa za kubomolewa kwa majengo yaliyojengwa bila kufuata taratibu za ujenzi zinazozingatia Mipango-Miji, Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza hili kushirikiana na Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiria Majenzi pamoja na wataalamu wa Mipango-Miji kuhakikisha kuwa vibali vya ujenzi vinatolewa kwa Wakandarasi wenye sifa na waliosajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu kuongeza juhudi katika kuzisimamia Bodi zake zinazohusika na sekta ya ujenzi, ambazo ni Baraza la Ujenzi la Taifa, Bodi ya Usajili ya Wahandisi, Bodi ya Usajili Wakandarasi, Bodi ya Usajili ya Wakadiria Majenzi pamoja na wataalamu wengine wa Mipango-Miji ili kujenga uhusiano mzuri wa kikazi baina yao ili kazi za sekta ya ujenzi ziwe za viwango na ubora unaokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna mabadiliko ya kila mara ya sayansi na teknolojia katika sekta zote, Kamati inawashauri Wakandarasi na Wahandisi kujenga utamaduni wa kujiendeleza kila mara ili kwenda sanjari na mabadiliko katika fani zao. Kamati inalikumbusha Baraza la Taifa la Ujenzi kuwa lina jukumu la kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wadau wa ujenzi kwa utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Baraza la Taifa la Ujenzi hupata takribani asilimia 50 ya mahitaji yake ya kifedha kutoka Serikalini na kutoka vyanzo vyake vya ndani (*Advisory fees*) na ili kuliwezesha Baraza hili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri kuwa Baraza liimarishwe kifedha ili liweze kujiendesha na kuiendeleza sekta ya ujenzi. Kamati inapendekeza kuwa, kwa mfano, namna nyingine ni kuliwezesha Baraza la Taifa la Ujenzi kupata mapato kutoka *Skills and Development Levy (SDL)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa moja ya vigezo ambavyo hutumika kupima uwezo wa Wakandarasi na Wahandisi kabla ya kupewa kazi hasa kwenye miradi mikubwa ya ujenzi kwa kuangalia ni miradi mingapi wamefanya, Kamati inashauri kuangalia uwezekano wa kuwapa kipaumbele Wakandarasi na Wahandisi Wazalendo kazi za ujenzi pale wanapokuwa wamekidhi masharti. Hii itawawezesha kufikia vigezo vya kupewa miradi mikubwa, ikizingatiwa kuwa ushindani mkubwa unatazamiwa kuwepo katika Jumuiya na baadaye Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa migongano inayoweza kujitokeza au ambayo imekwishajitokeza, kuna umuhimu wa kila Baraza ama Bodi za ujenzi kufanya kazi kulingana na mipaka yake ya kisheria. Kamati inashauri kuwa, sheria zinazounda Bodi zote zinazofanya kazi zinazolingiliana au kutegemeana ziangaliwe upya. Hii itasaidia kuondoa urasimu na migongano inayoweza kujitokeza kwa Bodi hizi kuwa na majukumu na mamlaka yanayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa wito kwa wadau wote wa sekta ya ujenzi, kutoa ushirikiano na taarifa zitakazoiwezesha Bodi hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari na Mheshimiwa Dr. Makongoro M. Mahanga, Naibu Mawaziri wa Miundombinu, Dr. Enos S. Bukuku, Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu, Ndugu Omar A. Chambo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu, pamoja na wataalamu na watendaji wote wa Wizara hii walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina pale yalipohitajika.

Pia napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Johnson P. Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru wadau wote niliokwisha wataja hapo awali kwa ushiriki wao katika *Public Hearing* na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, ambao walishiriki kikamilifu katika kuujadili kwa ufasaha na kuuboresha Muswada huu. *Schedule of Amendment* ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Wajumbe wa Kamati hii. Naomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohammed H. Missanga, Mwenyekiti na Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Makamu Mwenyekiti. Wafuatao ni Wajumbe wa Kamati hii nao ni Mheshimiwa Khadija S. Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Pascal C. Degera, Mheshimiwa Bakar S. Faki, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella na Mheshimiwa Dr. James A. Msekela.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Sigsfrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Hafidh A. Tahir, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi pamoja na Mheshimiwa Felix Kijiko, ninayesoma taarifa hii hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru

Makatibu wa Kamati hii Ndugu Justina M. Shauri, Ndugu Zainab A. Issa na Ndugu Michael Chikokoto kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu na kujadiliwa Bungeni. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. MHE. SHAMIS BAKARI FAKI): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi wa mwaka 2007 (*National Construction Council (Amendments) Act, 2007*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5) (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba Muswada huu ulinipata tabu sana katika maandalizi ya kuuchangia. Hii ni kutokana na sababu ya kwamba takriban siku tatu sasa umekuwa unaingia Bungeni na kutoka mithili ya *piston* kwenye *engine*, tunaambiwa ulikuwa haujaiva. Hata hivyo, nitajitahidi kuchangia machache kwa nia ya kuuboresha. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wao kwa kuutayarisha Muswada huu na hatimaye kuuwasilisha hii leo kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 3 cha Muswada kinachofuta na kuweka kifungu kipya cha 4(f) kilicholetwa katika Jedwali la Marekebisho, kinalipa kazi Baraza kwa kuandaa na kutunza orodha ya miradi na taarifa zote zinazohusiana na Tasnia ya ujenzi. Kifungu hicho kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(a) kinachomtaka mtu yeyote anayejihusisha katika shughuli za ujenzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa gharama zake mwenyewe kutoa taarifa zinazohusiana na shughuli za ujenzi kwa Baraza kwa muda ambao utakuwa umepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya kawaida tu maana ya vifungu hivyo inachanganya, na inafanya wahusika katika Tasnia hii ya ujenzi washindwe kuelewa wanawajibika kwa nani. Hii ni kwa sababu Tasnia ya ujenzi ni pana na inahusisha asasi nyingine zilizoundwa kwa mujibu wa sheria za Bunge. Kambi ya Upinzania inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusiana na vifungu hivyo viwili na uhusiano wake kwa wale wote waliomo katika Tasnia hii ya ujenzi na asasi zingine kama *CRB*, *ERB* na *AQRB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4 cha Muswada kinachokifanyia marekebisho kifungu cha 5 cha Sheria iliyopo katika Kifungu cha (b) kinachooongeza kifungu kidogo cha (2) kinasema, nanukuu: “*the Council shall provide leadership and be a focal point or sector co-ordination of all the institutions.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zote zinazoshughulika na uangalizi wa masuala ya ujenzi zimeanzishwa kisheria na katika sheria za uanzishwaji wa Taasisi hizo hakuna vifungu vinavyoagiza kuwa zitalazimika kupokea mwongozo katika utekelezaji wa shughuli zao toka Baraza la Taifa la Ujenzi. Kama kuna ulazima wa kifungu hiki kuwepo, ni vyema basi Serikali izifanyie marekebisho sheria zilizoanzisha asasi kama vile *CRB*, *Association of Quantity Surveyors Registration Board (AQRB)* na *ERB*. Vinginevyo ni kuleta mtafaruku usiokuwa na sababu katika Tasnia hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa machache hayo, na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, angalau wachangiaji wapo, lakini wakiongezeka siyo vibaya. Nitaanza na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na Mheshimiwa Fuya Kimbita ajiandae.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu. Lakini kama walivyosema wasemaji walionitangulia na mimi ningependa kutumia nafasi hii kuwapongeza viongozi wetu wote wa kitaifa waliochaguliwa kutuongoza katika Chama chetu Tawala. Vilevile na wewe nakupongeza kwa kurudi tena katika Kamati Kuu na nakutakia kila la heri. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia uniruhusu niseme ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kwa upendo wao kwa namna walivyomchangia na kumpa kura binti yangu. Naomba wafikishe salamu kwa wapiga kura wote nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano kidogo, gazeti moja sitaki kulitaja, kila siku wakiwa wanaandika jina la yule mgombea wananiandika mimi kwamba mtoto wa kigogo atapata shida sana kupita baba yake siyo maarufu tena. Lakini mtoto aliposhinda wamefuta jina langu wameandika Vailet Mpogoro, kwa sababu wanaona haya kuandika. Hayo ndiyo magazeti yetu! Kwa hiyo, wamepata aibu wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu ya kusema. La kwanza ambalo ningependa kuchangia lipo katika Muswada wenyewe kifungu cha 7(c) na (e). Vifungu hivyo vyote vinazungumzia kuhusu mafunzo, na mimi nilikuwa nataka kushauri kwamba Taasisi hizi tunazozitengeneza ambazo kazi zake nyingi ni *professional*, nafikiri tungeweka mkazo mkubwa sana katika kufundisha *capacity building*. Sababu hii ndiyo inayotufanya mambo yetu yasiende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi ninamfahamu Mtendaji wa sasa wa Chombo hiki. Nataka nitumie nafasi hii kumpongeza kwa sababu kwa kuwa anafanya kazi kwa uaminifu mkubwa sana na amefanya kazi nzuri sana katika kipindi chake. Nina matumaini Serikali itamfikiria hata katika mabadiliko maana kwa kweli amefanya kazi nzuri. Sasa uwezo wa chombo chenyewe ni jambo la kwanza. Lakini vilevile mimi nadhani kungekuwa na programu pia maalumu ya kuwa na uhusiano wa kimafunzo kati ya chombo na hao wajenzi wadogo. Kwa sababu katika nchi yetu kwa mfano, ukitazama orodha ya *contractors* hao wadogo uwezo wao ni mdogo sana, na ndiyo maana kazi hizo kubwa hawapewi, zinapewa kampuni kubwa kutoka nje.

Mara nyingi imekuwa vigumu sana kuwaunganisha. Mimi natoa wazo kwamba Wizara ingetazama namna ya kuwaunganisha hao ili kwa umoja wao na kujenga nguvu ya makandarasi wadogo hao waweze kupata kazi kubwa ambazo zinafanyika katika nchi yetu. Kwa vyovyote vile lazima tutengeneze programu ya kujitosheleza au kuanza kujitegemea kwa kuwa na makandarasi watanzania wenyewe, na hii inatakiwa iwe ni programu ya chombo hiki na Wizara yenyewe. Hilo ndilo pendekezo langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ambalo ningependa kulisemea ama kumekuwa na kuona haya ama ni uwezo mdogo. Mara nyingi hao makandarasi wadogo wanapooomba kazi wanaweka viwango vya chini mno kiasi ambacho hawawezi kumudu kutimiza kazi walizopewa vizuri, na wengi wao hawana vyombo. Vyombo vyote vya kufanyia kazi lazima waende wakakodishe kwa makandarasi wakubwa. Kwa maana nyingine utagundua kwamba makandarasi hao wadogo wanafanyia kazi makandarasi wakubwa ambao ndiyo wana vyombo vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili jambo naomba nalo litazamwe namna ya kuwajengea uwezo watu wetu. Vyombo hivi vinavyotoa mikopo vingeweza vilevile vikawa na programu ya kukopesha watu wetu zana za kufanyia kazi. Hata Wizara yenyewe ingefikiria. Kwa mfano, zamani nakumbuka kule kwetu Rukwa *NORAD* walikuwa wameanzisha kituo cha zana za barabara na Mbeya sasa kipo kizuri tu. Sasa vyombo kama hivi vingeanzishwa na Serikali ili kuwasaidia kupata nguvu hao makandarasi wadogo ambao wenyewe hawawezi kununua zana za kisasa. Hilo ndilo nilikuwa napendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilieleze ni mambo haya ya *corruption*. Zamani niliwahi kusema na nataka nirudie maneno ambayo niliwahi kusema. Nilisema hivi, Rais wa nchi anaweza akakemea rushwa, lakini watendaji waandamizi kwa mfano, Mawaziri, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, inakuwa siyo sawa. Kwa mfano, kama *Inspector General* akisimama akasema Jeshi lake kuna wala rushwa, mimi naona kuna kasoro. Kwa sababu lazima yeye achukue hatua, yeye hawezi kuhutubia na kukemea rushwa, lazima achukue hatua kwa wale anaojua wanakula rushwa.

Vilevile kwa mfano katika Wizara kama Wizara fulani inalalamikiwa ni juu ya Waziri wa Wizara hiyo kudhibiti na kuchukua hatua kwa watu wanaosemwa wanakula

rushwa. Maana haiwezekani kila mtu akisimama analalamikia rushwa, rushwa, sasa nani atadhibiti na nani ataondoa rushwa kama kila mtu anasimama ananung'unika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba ingekuwa ni vizuri kila mtu achukue jukumu mahali pale pa kazi kuondoa na kudhibiti mambo ya rushwa. Haiwezekani tukadhani kwamba rushwa inayozungumzwa hapa ni ile ya kutegeshea, lazima tuanze kufikiria mbinu nyingine ya namna ya kushughulikia rushwa. Kwa sababu kama kwa mfano, mimi nimepewa kazi ya Serikali, mshahara wangu ni shilingi milioni moja na laki tano, halafu najenga nyumba ya milioni 300 nimezipata wapi? Maana mshahara wangu haufanani na kujenga nyumba ya milioni 300 na sikukopa zimetoka wapi? Mimi napata mshahara wa shilingi 1,000,000/= lakini naendesha Benzi, nimeipata wapi Benzi na sijafanya biashara? Nategemea mshahara wangu huo huo, sasa na hiyo yenyewe ni kasoro, inatosha kujua kwamba hapo kuna jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza au natoa ushauri kwa Serikali kwamba kila mtu mahali pake pa kazi achukue jukumu la kudhibiti rushwa, hakuna haja tena ya kunung'unika wala kuhutubia kwamba kuna rushwa. Kazi hiyo, tunaweza kumwachia mtu mmoja kukemea Mheshimiwa Rais tu. Wengine kila mtu achukue hatua mahali pake pa kazi, kwa sababu kila mtu amepewa madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii angalau nitoe yangu machache kuhusu Muswada huu wa *NCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nilishatoa pongezi na pole jana sina haja ya kurudia tena huko. Naona nijikite moja kwa moja katika mchango wangu ambao utakuwa ni kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli wa mambo hii *National Construction Council* imepitwa na wakati na huu ndiyo ukweli. Chombo hiki hivi sasa pamoja na haya mabadiliko tunayofanya basi hayajasaidia na yamezidisha utata na utata ni mkubwa zaidi na hakuna siri. Tunaelewa namna gani ushahidi wa utata huu, wiki mbili za Vikao vya Kamati Dar es Salaam kujadili Muswada huu hazikutosha, umeingizwa kwenye *Order Paper* mara tatu hazikutosha mpaka juzi, jana na leo, sasa hii yote ni ushahidi kwamba Muswada huu una utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vifungu vinavyoonyesha ushahidi huu. Ukweli hii *National Construction Council* ingefutwa au katika marekebisho ikawa tuna Bodi hii labda inashughulikia na *Policy Making* kwa ajili ya Bodi nyingine ambazo zipo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitazama *information* yake tangu mwaka 1979, tutazame *performance* yake imefanya nini. Kwa sababu *performance* ya *ERB*, *CRB* na *AQRB* inajulikana na zinaonekana. Lakini *performance* ya *NCC* iko wapi? Mheshimiwa

Waziri anaweza akatueleza *performance* yake iko vipi. Mpaka leo tangu mwaka 1979 bado Ofisi yake ipo Dar es Salaam tu wakati wengine waliokuja baadaye miaka 1997 tayari wamekwishasambaa nchi nzima takriban wamechukua nafasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Muswada huu kwa kweli una utata pamoja na haya marekebisho. Kwa mfano, tukiangalia katika kifungu hiki tunacho-*amend section 4*, tunafuta *section 4* na kuingiza *section 2* ambayo kuna maneno hapa katika kifungu (f) *amendment* ya mwanzo na kifungu (f) kinazungumzi: “*provide and promote the documentation and dissemination of construction industry related information including establishment of a Register...*” Sasa *CRB* wanacho kifungu hicho na wao ndiyo wana-*register*. *ERB* hivyo hivyo, halafu leo na *NCC* iwe hivyo hivyo, na sasa hivi imefanyiwa *amendment* tena imeondoshwa. Kwa hiyo, hakutokuwa na ku-*register*.

Lakini hayo marekebisho mengine yaliyofanywa bado utakuwa kuna kitu “*compile and maintain a list of projects and promote the documentation and dissemination of information related to construction industry.*” Bado kuna chombo huko huko katika Wizara ambacho kinafanya kazi hiyo.

Sasa *Building Research Unit* ipo na imeundwa kisheria ipo katika Wizara hiyo hiyo inafanya kazi hiyo ya *research* na ipo *compile documentation* na *information*, ni nini hizo *research* hiyo hiyo. Kwa nini kuwa na vyombo viwili katika Wizara moja na wao hao wapo. Hii ni kujichanganya na kuongeza mzigo ambao hauna faida kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitazama tunafuta kifungu cha 4 na tunaweka kifungu cha (3) ambacho kazi zake zilizotajwa katika (3) (a) na (b) na (3) (d) ni pamoja na kutoa mafunzo. Lakini *ERB* wanatoa mafunzo, wanafanya semina, wanafanya kongamano ambazo zinaonyesha taaluma za kileo za dunia katika sekta hii ya *Industry* ya *construction*. *CRB* vilevile wanafanya hivyo, *AQRB* wanafanya hivyo, sasa haya ni mafunzo gani hayo wanayotaka kutoa, hii tunajiingiza tunaji-*complicate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli mimi nisingependa kuendelea na vifungu vingine kwa sababu tungeweza kutoa ushauri wa vifungu tulivyofuta na kuongeza vingine, lakini naona tunazidisha utata. Kuna hili suala la kwamba lazima labda nikisome kile kifungu. Hiki tulichosema: “*compile and maintain a list of projects and promote the documentation and dissemination of information...*”

Kuna kifungu cha adhabu, sasa ikiwa ni *contractor*, basi *CRB* wapo juu yao, hizo *information* zote wanatoa huko. Ikiwa ni *Consultant ERB* wapo juu yao, hizo *information* zote wanatoa huko. Sasa ikiwa ni *investor* tu amekuja kutoa *information* hizo kuna sehemu nyingine nyingi za kutoa *information* kiasi ambacho tukiziongeza za ziada tunaji-*complicate* vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ikiwa *investor* akija basi anatoa *information TIC*, *investor* akija inategemea anatoa *information* kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ametoa *information TRA*. halafu sasa unaongeza na huko

atoe *information*. Sasa ndiyo pale *investors* wakati mwingine wanapotukimbia kwa mizunguko hiyo. Wakati vyombo hivi vyote ni vya Serikali, *information* ikishatolewa sehemu moja inaweza ikaenda sehemu nyingine. Kwa nini watoe *information* zote hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo, kuna hii sehemu ya kuhusu mabadiliko ya kifungu cha 6. Kuweka cheo cha *Chief Executive Officer* ambaye atachaguliwa na Mheshimiwa Waziri. Kama hii haifutwi na ninajua ndiyo matatizo ya hapa, lakini Waziri asiweze kuchagua huyo *Chief Executive Officer* moja kwa moja.

Labda ningeomba Mheshimiwa Waziri afanye mabadiliko angalau aweke neno kwamba Waziri akishirikiana na *CRB*, *ERB* na vile vyombo vingine kwa ushauri wa vyombo hivyo ndiyo achagulie mtu huyo, kwa sababu hao ndiyo wanaojua *competent person* ni yupi na wanajuana mwenye uwezo wa aina gani ni upi. Kwa hiyo, Waziri apate ushauri wa hao ndipo achagulie huyo *Chief Executive Officer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kule kusuasua siyo sababu ya ubora au Muswada kutokuwa bora. Sasa hivi hata kanuni zetu mpya tutakazoiweka tutapenda kupata nafasi kubwa ya wadau au “*Public Hearing*.” Kwa sababu sheria zetu tukizitunga kama tunajitungia sisi wenyewe humu ndani zikitoka nje haifai, basi inakuwa siyo sheria.

Kwa hiyo, kila inapowezekana tukipata wadau wanaotaka kushirikiana na sisi tupo tayari kuahirisha Muswada ule kama tulivyofanya ili wapate kushiriki. Tukimaliza kutunga kanuni zetu utaratibu utakuwa mzuri zaidi wa kuwashirikisha watu wengi zaidi kuweza kujadili Miswada yetu kabla haijaingia Bungeni. Kwa hiyo, tunaendelea na Msemaji anayefuatia Mheshimiwa Futa Kimbita na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ajiandae.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu. Labda mimi niende haraka haraka, niwapongeze Wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa na nzuri iliyoanyika ya Mkutano ulioleta mambo mazuri, na niwapongeze wote waliochaguliwa ikiwa ni pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Miundombinu pamoja na wengine wote nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana katika ujenzi. Juzi hapa tumezungumzia mambo ya *Registration of Engineers*, sasa leo tunazungumzia hao wenzetu ambao ndiyo Bodi ya Ujenzi. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge waliokwihatangulia kusema, ukiusoma kwa undani Muswada huu utaona kuna shida, saa nyingine unakuwa na shida unashindwa kuisema wazi ilimradi twende tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Muswada huu una shida. Shida ninayoiona ni kwamba kuna kuchanganya kidogo wa mambo. Hizi kazi za wenzetu wa *NCC*, tayari kuna hizo Bodi zinazofanya hizo kazi. Ninachomaanisha nini? Hii Bodi yetu ya *NCC*

iliundwa tangu mwaka 1979, imekuwepo kwa kipindi hicho, kwa bahati mbaya natumaini haikusikika vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka 1997 zikaundwa Bodi kwa mfano, *Contractor Registration Board*, hii Bodi ya Makandarasi, *Engineers Registration Board*, *AQRB*, hao wenzetu wamefanya kazi kwa haraka sana na tena nitumie nafasi hii kuwapongeza wameenea nchi nzima. Wamefanya kazi katika ule mtindo tunaoita *digital*.

Sasa wataniwia radhi kidogo nikisema wenzetu *NCC* walienda katika *System* ya *analogy*. Sasa hizi Bodi zimeenda ki-*digital* zimefanya kazi kwa haraka papo kwa papo. Sasa tunavyokuja kufikia wakati kama huu nadhani wenzetu wameshituka kwamba kasi ilikuwa imewapita. Kwa hiyo, inabidi sasa waje na hayo masuala mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi maoni yangu naomba sana kuwepo na mipaka katika hizi Taasisi. Taasisi zinazofanya kazi za *regulation* ziachwe zifanye hizo kazi. Hao wenzetu wa *NCC* nadhani wao ni katika kufanya *promotion*. Kwa sababu kuna baadhi ya vifungu hapa vimekwishazungumzia, Ibara ya 3. Hii kazi inayofanywa pale katika hiki kifungu cha tatu hapo, tayari kuna Bodi ya Usajili ya Makandarasi, wanafanya ile ku-*compile list*.

Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba hao wenzetu wa *NCC* wasingezipata hizo taarifa moja kwa moja kwa wenzao wa *CRB* ikawa na maana ya kutoa mkanganyiko wa kutoingiliana katika kazi, na hao wenzetu wa *NCC* ili tuwaache wafanye kazi hizo za *promotion*. Lakini niwaombe sasa ule utafiti wa nje usifanyike mno ila ufanyike wa hapa ndani.

Tumeshuhudia kuna jengo lilianguka kule Kariakoo miaka ya nyuma kidogo. Kuna jengo limelilianguka siku za hivi karibuni Keko hata Waziri Mkuu ikabidi achukue hatua za dharura kufanya uchunguzi. Sasa ningependa hao wenzetu wa *NCC* kazi zinazofanywa na hizo Bodi ambazo tumezishuhudia kwa vitendo ni vizuri waachiwe hao wenzetu wazifanye wenyewe pasipo kuingiliwa, kwa maana ya kuheshimiana katika mipaka ya kazi katika hizi Taasisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kile kifungu cha Ibara ya 10, pamoja na hii karatasi ya mabadiliko iliyokuja sasa hivi, *page 5* wanazungumzia kuunda *Council*. Tunaposema ni watu tu wanaotoka kwenye hii *industry* ya ujenzi hapa pasipokuwepo na wale ambao ndiyo wanao-*regulate*.

Pendekezo langu lingekuwa pale tunaposema kwamba: “*seven other members representing the private sector appointed by the Minister drawn from categories of professional groups or institutions on the basis of professional competence and experience as follows:-...*” Wametaja *Contractors, Architects, Engineers, Quantity Surveyors, Manufacturers* na hao wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza badala ya kusema ni *Contractors, Architects, Engineers, Quantity Surveyors*, wawepo wawakilishi wanaotoka kwenye zile

Bodi ambao ndiyo wanaowasajili na kuratibu utendaji wao. Kwa sababu anaweza akatokea *Architect* ambaye hajasajiliwa akawa kwenye ile Bodi, atakuwa ni tofauti sana akiwemo na mtu ambaye ametoka ndani ya Bodi anayefanya lile jukumu la kuwasajili hao watu na kuwaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi pendekezo langu hapa lnienda moja kwa moja, ni kwamba wapo viongozi wa hizi Bodi labda ndiyo wangukuwa *mentioned* hapo. Kwa mfano, kwenye *Contractors* awapo Msajili wa *Kandarasi*, Msajili wa *Architects* na *Quantity Surveyors*, Msajili wa *Engineers* awe ndiyo anaingia kwenye ile *Council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba tutazidi kumwongezea mtanzania mzigo. Tunaposema anapewa muda wa kwenda kusajili mradi awe ni *contractor*, labda tafsiri yake ni kwamba asipotimiza ule wajibu maana yake kuna faini au kwenda kusajili kule kwao labda kuna kulipa *fees* fulani.

Ukiwa kama *contractor* ile *fee* huiachi kwako. Wewe *contractor* unaipeleka mbele zaidi kwa *client*, ina manaa tunazidi kum-charge yule Mtanzania. Sipingi *NCC* kuwepo nasema ipo, lakini mipango ya kazi iwepo kati ya *NCC* na hizo Bodi nyingine zinazofanya hizo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mkubwa kazi nyingi katika *industry* ya *construction* zinafanywa na hizi bodi zetu tatu, *Contractor Registration Board*, *Engineers Registration Board*, *Architects and Quantity Surveyor Registration Board*, wanafanya kazi nzuri sana katika *industry* ya ujenzi. Wenzetu wa *NCC* labda sasa iwe ni wakati mwingine tukija mbele ya safari tuangalie zaidi kama tutaweza kuwaingiza kwa sababu na wale ni mainjinia tu, wanaingia katika hizo bodi itawasaidia kutoa ukiritimba.

Shida ninayoiona hapa ni kwamba tutatumia muda mwingi kwenda kufanya mambo ya usajili kwa vitu ambavyo vimeshasajiliwa na bodi zinazohusika, na matokeo yake tunazidi kucheleweshana, na mimi nikizingatia kwenye Chama chetu Chama Tawala tunasema Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Sasa hii itakuwa tunarudi nyuma sana na tunazidi kupoteza muda kwa maana ya urasimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nitaendelea kusisitiza siku zote dunia ya leo na ili tuweze kwenda pamoja na wenzetu Ulimwenguni ambapo kijiji kimekwishakuwa ni kimoja. Unaweza tu ukaingia kwenye Tovuti ya hizi Bodi ukapata taarifa unazozihitaji kama wenzetu wa *NCC* watazihitaji, badala ya kusema kwamba lazima watu waanze kwenda kwa miguu mpaka labda kufika ofisini kwao kupoteza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tusiendelea kupoteza muda zaidi twende *digital*, wafunge ile Tovuti watapata *information* wanazozihitaji pasipo kuwasumbua sana hao wenzetu wanaotakiwa kwenda kwenye Ofisi zao labda kusajili hizo kazi pamoja na kufanya mambo mengine.

Wao tuwaachie hayo mambo ya kufanya utafiti, na huo utafiti naomba ufanyike zaidi hapa nchini. Nadhani ukienda pale *NCC* utafiti mwingi labda unaweza ukawa ni wa nje zaidi kushinda wa hapa ndani. *I am very much sorry to say this*, lakini ndivyo hivyo hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi huo ndiyo ulikuwa mchango wangu kwamba tuiheshimu ile mipaka, lakini ninatumaini huenda muda si mrefu tukalazimika kuja kuangalia upya majukumu ya wenzetu wa *NCC*. Kutokana na dunia na mabadiliko yaliyopo na wenzetu hao wanavyofanya kazi zao vizuri; je, wanao umuhimu wa kuendelea zaidi kuwepo? Kwa sasa hivi sisemi kwamba tuwaondoe kama mwenzangu alivyotangulia kusema moja kwa moja, hapana! Wawepo, tuheshimiane katika mipaka tuje tuangalie mbele ya safari kwamba majukumu yanayotekelezwa na *NCC*; je, tuyaingize kwenye hizo bodi zinazohusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa ni mchango wangu. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo. (*Makofi*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ingawaje uelewa wangu kwenye mambo haya siyo mkubwa sana, lakini nimejitahidi kuusoma Muswada huu kwa kadri ambavyo nimeuelewa. Baadhi ya niliyoyakusudia kuyauliza au pengine kuyachangia yamekwishasemwa. Kwa hiyo, labda niende moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NCC* kwa kweli kabisa mimi kama baadhi ya wenzangu walivyosema hata mimi katika kupita pita ambapo nimekaa sana Serikalini na kwingineko, hata kwa kweli si kitu ambacho ninakisikia mara kwa mara na shughuli zake. Mimi nilikuwa nauliza; je, hao watu data zipo, hivi ukienda *NCC* sasa hivi unaweza ukasema ninataka labda *architects* wangapi au ukataka takwimu mbalimbali je, wanazo? Hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini je, hizo tafiti wanazofanya na taarifa zinapatikana wapi? Maana yake nyingi utazikuta labda ukiingia kwenye Tovuti na katika maeneo mengine au utazikuta kwenye magazeti mbalimbali ambayo ni muhimu. Lakini hii hapa sioni kabisa wapi ambapo nimeweza kuona *research* hizo ambazo kwa kweli ni za muhimu sana kwa wakati kama huu.

Vile vile nilitaka kujua hata hizo zilizoko maana yake naambiwa kwamba huwa zinafanyika, je, zinafanyiwa kazi? Kama zinafanyiwa kazi ni kazi zipi maana yake kuna mapungufu mengi tunaona maeneo mbalimbali. Lakini nikisoma huu Muswada naona *functions* nyingi walizonazo ni katika hayo ambayo kwa kweli mara nyingi unaona kwamba hayajafanyiwa kazi, sasa nauliza zinafanyiwa kazi? Je, taarifa zinatolewa mapema? Kutokana na kuusoma huu Muswada kwa Kiingereza changu kidogo nimeelewa kwamba hawa watu pia wanatakiwa kutoa maelekezo hasa kwa wananchi na mambo mengine.

Nitolee mfano mdogo hapa Dodoma, sasa hivi kunajengwa vyuo vikuu, watu wanajenga nyumba, mji unapanuka na kadhalika. Sasa mimi nilitegemea chombo kama hiki kinatakiwa kifanye kitu kama kuelewa kwamba je, sehemu ya kuhifadhi saruji ipo na kama ipo inatosheleza kiasi gani ya *storage* pale na je, inatosha kwa *consumption* ya Dodoma kwa wakati kama huu na kutoa mwelekeo? Ni vyema kabisa watu kama hawa wakawa wanatoa taarifa maana yake nitoe tu mfano, si vyema kungoja mvua inyeshe halafu unasema mvua imenyeshwa wakati wote tumeona mvua imenyeshwa. Ni vyema ukatoa taarifa na tahadhari mapema watu wakajiandaa. Lakini ndio nasema pengine mimi kama Beatrice siwezi kujua labda wengine wanafahamu, lakini kwa kweli niliona na mimi nichangie kwenye hili.

Vile vile hapa nilikusudia kuuliza *NCC* ipo mikoani, kwa sababu kutokana na *functions* zake ambazo nimezisoma hapa na ambazo zimeongezewa nimeona kwamba hii *NCC* nimepata kuelewa baada ya nadhani hotuba mojawapo kusomwa kwamba wako Dar es Salaam tu, je, huku mikoani vipi? *NCC* tumeambiwa imeanza mwaka 1979 mpaka leo tumeshindwa kupata huduma hii huko mikoani au wana-*operate* kutokea Dar es Salaam, kwa hiyo, hili pia nilitaka nilifahamu.

Lakini vilevile nauliza je, wako watumishi wa kutosha katika Baraza hili? Maana yake jambo lingine inaweza ikawa hakuna watumishi labda wenye uwezo, lakini naamini wapo watu wenye uwezo ambao wamesoma, *researchers of the high stockholder* wapo. Lakini sijui kama inao wa kutosha. Je, kama wapo, wapo muda gani pale kwenye ile? Kwa utafiti mdogo niliufanya baada ya Muswada huu kuahirishwa aharishwa nimegundua kwamba hata Mtendaji Mkuu wa *NCC* ameanza kazi mwaka 1979 wakati inaanza *NCC* mpaka leo. Kwa heshima kabisa *with due respect* anafanya kazi yake pengine vizuri, lakini pia nadhani uzoefu umetuonyesha kwamba mtu anapokaa mahali muda mrefu ana *tendency* hata baadaye pengine na *staff* pia wamekaa muda gani na kama basi mnaona vipi labda tufanye mabadiliko kidogo ili angalau tulete *dynamism* na unajua mabadiliko mara nyingi yanaleta chachu mpya.

Sasa lakini *with due respect*, sina nia mbaya, nasema pengine wamefanya kazi yao vizuri mimi ndio sielewi, lakini ni vyema pia kuangalia watu wakikaa muda mrefu, nadhani hili limejionyesha mara nyingi na katika maeneo mengi tumekuwa tukiangalia kuweza kubadilisha kidogo. Kamati hapa imependekeza wapewe bajeti ya kutosha na mimi kwa kweli nilikuwa nauliza labda pengine hawana bajeti ya kutosha, lakini hata hiyo kidogo wanayopata labda pengine niseme tena wanafanyia nini? Maana yake tupendekeze wapewe bajeti, tukiwa tunaona, lakini kwa wale ambao wanafahamu hata michango yao na nje tulivyokuwa tukiulizauliza na kutaka kupata taarifa hata wao wanasema hakuna mengi makubwa yanayofanyika. Sasa tusikimbilie kwenye bajeti labda iwe mojawapo lakini kwanza tuone tatizo ni nini, ni hiyo *duplication of roles* au pengine kuna matatizo mengine. Mimi kwa kweli nilikuwa naomba sana kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikiangalia *item 3* pale iko kwenye *amendment* inasema: “*Any person who contravenes the provision of sub section (1) commits an offence and upon conviction shall be liable to a fine not exceeding one*

million shillings”. Sasa nasema hii inaletwa Bungeni kuja kubadilishwa je, tutaleta mara ngapi? Thamani ya shilingi inakwenda chini na makosa pengine yatakuwa makubwa.

Kisheria haina matatizo, kwa nini tuiseme: “*Shall be liable to a fine not less than one million.*” Kwa hiyo, pale ambapo fedha hizi zina-*differentiate* wanaweza wakasema tu wanaongeza bila ya kuleta tena hapa kuliko kuweka *fixed* halafu kesho mnakuta ile *one million* imekuwa kama sasa hivi ilivyo shilingi laki tano. Nilikuwa tu nauliza kama kisheria haina sababu basi labda tungeangalia tuweke kwa utaratibu mwingine ili kwamba sio lazima tena ingoje kuletwa Bungeni ili iweze kubadilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kwenye suala la Wajumbe wa Baraza, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kwamba wanakusudia kuwa na Wajumbe saba kutoka kwenye umma halafu na saba kutoka sekta binafsi. Sasa napendekeza hapa mara nyingi inasahaulika inakuwa sekta binafsi halafu jinsia haizingatiwi, naomba sana ama itaweka kipengele au kama sio iweke kipengele wale watakaofanya uteuzi basi wazingatie na jinsia. Ni hayo nilitaka kuchangia na mimi nashukuru. (*Makofi*)

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi pamoja na viongozi wote waandamizi katika chama waliochaguliwa kwa kishindo katika Mkutano Mkuu uliofanyika *week end* hii. Napenda nichukue nafasi hii pia nikupongewe wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuingia katika Halmashauri Kuu ya Taifa pamoja na Kamati Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwapongeza wenzangu Wabunge humu ndani pamoja na Mawaziri ambao wamechaguliwa kuingia kwenye *NEC*, naamini kwamba Mwenyezi Mungu ataendelea kuwabariki na kuwapa busara ya kukiendeleza Chama cha Mapinduzi ili kiendeleo kutawala kwa amani katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Watendaji wake pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta hii *amendment bill* katika Baraza hili la Ujenzi la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi zaidi ila ninayo machache ya ujumla ya kuchangia kwa nia ya kuboresha tu. Kwanza nilikuwa na *big concern* ambayo nafikiri imekuwa *addressed* na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwamba katika Mabaraza yote ambayo tumepitisha hapa sisi kama Wabunge hususan Wabunge Wanawake tumesahau kuomba Serikali iingize kifungu kinachosema kwamba: “Katika Wajumbe hao kwenye *composition* kuwepo angalau mwanamke mmoja kimaandishi”. Kwa sababu tukisema tunaamini kwamba atakayeteua atafanya hivyo inawezekana akasahau.

Naamini kwenye Baraza hili tuna wanawake wengi tu mainjiniya, tuna wanawake *architects* ambao wanastahili kuwepo mle kwa sababu katika hii shughuli ya ukandarasi na ujenzi tuna wanawake ambao pia wamejitokeza kama makandarasi, wanafanya kazi. Tuna wanawake ambao wanahitaji kuwa *registered*, sasa nani atakayeangalia *interests* za hao wanawake katika hili Baraza? Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninaangalia maadili ya ujenzi ya makandarasi kwa kweli naomba kusema kwamba inaelekea hakuna maadili kabisa. Wengine wanafanya kazi yao kama biashara wakisahau kwamba wao kama *professionals*, wanawajibika kuhakikisha kwamba kuna usalama wa raia na wananchi kwa kufuatana na aina ya kazi wanazozifanya. Naomba nitoe mfano kuna mainjini wengine ambao wanadiriki kuwasaidia *contractors*, naomba kusema tu kwamba sasa hivi tuna *trade liberalisation* katika nchi hii. Kwenye hiyo, biashara na biashara ya ukandarasi pia imeingia humo.

Unamkuta mtu ni mkandarasi lakini bahati mbaya hajawahi hata kusoma *physics* kwenye darasa la sita na saba lakini ni mkandarasi. Ukimwuliza wewe ndugu yangu inakuwaje sasa umekuwa ni mkandarasi na tenda unapata. Anakwambia kwamba mimi ninasimamiwa na injinia ambaye ana *professional qualifications* na huyu injinia ambaye ana *professional qualifications* hafuatili kwamba huyu ambaye amemsimamia ili aweze na yeye ana-*float* tenda apate fedha kwamba kazi anayoifanya inaendana na maadili ya uinjini, hawafanyi hilo. Matokeo yake ni kwamba tunaanza kuona kama majengo yanayoporomoka, tunaanza kuona barabara zinajengwa *sub-standard* ambazo zinaingiza Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mkubwa ni kwenye Halmashauri zetu. Barabara zinazojengwa na Halmashauri nyingi zinapewa makandarasi ambao tunasema sawa ni wazawa lakini *most of them they have no professions qualifications*, inakuwaje barabara inajengwa inakuwa kama tuta la kupanda viazi? Au ndugu zangu hamzoni hizo barabara?

Barabara inajengwa inasemwa ni ya changarawe lakini mvua ikinyesha basi yote inaporomoka na hakuna anayejali kwamba hapo kuna fedha za Serikali na jasho la wananchi ambalo linakwenda na maji. Je, kwenye Halmashauri zetu tunapo-*float* zile tenda ni nani anayetakiwa kuangalia kwamba kweli huyu anaye-*bid* hii tenda ana *qualifications*? Ni mtu anaitwa injinia wa Halmashauri.

Sasa huyu Halmashauri *against his registered*, lakini uadilifu wake uko wapi katika kuhakikisha kwamba kazi inayofanyika imekuwa ni kazi ambayo ina viwango? Haitarudiwa tena kujengwa mara ya pili kusudi kile kidogo Taifa ilichokuwa nacho kitakwenda kwenye kujenga barabara nyingine ili kuwepo na mwendelezo mzuri wa miundombinu ili kuleta maendeleo. Hilo ni swali ambalo sijui ni nani atakayelijibu lakini naamini sasa leo hawa ndugu zetu wa *NCC* pamoja na Wizara husika litaangalia kwamba mambo haya ya kudhamini watu kuwa makandarasi katika nchi yetu haitakuwa na mwendelezo tena itakuwa ni mwisho wake.

Mimi naamini kwamba tabia hii ya ku-*register* makandarasi ambao sio *professionals* ndiyo ambayo imechangia sana kuongeza chachu ya rushwa katika shughuli zote za ujenzi katika Taifa letu. Ndiyo kwa sababu unamkuta yule ambaye ni *professional* katika *bill of quantities* anapo-*bid* anatoa fedha nyingi na kiwango chake kinakuwa ni kikubwa kuliko yule ambaye ni *sub-standard*.

Sasa kwa sababu kuna mambo mengine ambayo hatuelewi kwa nini yanafanyika, hivyo unamkuta huyo ambaye ni *sub-standard* ndiyo anayepewa barabara halafu mwishoni ndiyo tunasikia kwamba mkandarasi amekimbia hatujui halipo. Sasa unapoangalia ni mkandarasi wa aina gani, ni mkandarasi ambaye sio *professional*. Kwa hiyo, naomba tuipe hii *professional ya engineering and construction* heshima yake kwa sababu ni watu ambao naamini wanasoma shule na wanasoma shule kuja kulihudumia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia niulize jambo moja ambalo sikuliona vizuri. Unapokuwa na *council* kama hii ni lazima pia basi iwajibike kuangalia kwamba wale ambao wanakuwa *registered* wanakuwa na uwajibikaji. Je, huo ufuatiliaji au *monitoring* unafanyika? Kwa mtindo huu kwamba *NCC* bado iko Dar es Salaam haiko katika mikoa ni kwamba hakuna ufuatiliaji.

Kwa hiyo, mimi ambacho ningependa kuomba ni kwamba kuanzia sasa basi *NCC* iweze ikajenga *in built mechanism* ambayo inaweza ikafuatilia ubora wa utendaji wa *professionals* ambao wanakuwa ni *registered* na wale ambao wanaingia kwenye hii biashara ya ukandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuona sheria ni *one thing* na kutekeleza *enforcement* ya hiyo sheria *is another thing*, tatizo letu sisi Watanzania ni kutunga sheria zikakaa kwenye *shelf*, tukatengeneza Bodi zetu zikakaa kule Dar es Salaam wakawa wanaendesha semina. Semina, sioni kwa nini wao waingie kwenda kuendesha semina na sio kutumia *other professional bodies* ambao wana utaalamu wa *engineering* kufanya hiyo kazi wao wakafuatilia na kuangalia kwamba sera ya ujenzi ya nchi hii inatekelezwa na inalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi sana ila ningependa tu kurudia kwamba *my concern* kwenye hii *council* ni *gender balancing* pamoja na maadili na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za makandarasi na *other contractors* ambao wamekuwa *registered* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii na mimi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii na mimi nichangie kwenye Muswada huu uliopo mbele yetu. Jana nilitumia nafasi hiyo kukipongeza Chama chetu kwa kuzidi kushamirisha demokrasia na kuwapongeza wote waliochaguliwa, naomba leo niende moja kwa moja kwenye Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu ambao nitamke (*declare*) hii *interest* na kusema kwamba huu Muswada una matatizo ndiyo maana umechelewa, sio kweli! Kama ulivyosema mwenyewe na mimi naomba nithibitishe kwamba huu ni Muswada ambao ni vitu vya kiutalaamu zaidi.

Msipokuwa waangalifu mkaleta haraka haraka muonekane mmekwenda haraka mnaongeza matatizo ndani ya nchi na ndani ya hii *profession at the end of the day management* yake itakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, kwa kweli tujitahidi kuwa *careful* tukajitahidi kuwahusisha watu wote wadau ili tuelewane na hii ndiyo ilikuwa sababu ya Muswada huu kuchelewa.

Mimi, kwanza niseme *NCC* ni chombo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ukisoma kwenye Muswada huu ukaangalia *functions* za *NCC* unaweza ukajua umuhimu wa sheria hii ambayo tunaipitisha leo. Sekta ya ujenzi ni moja ya sekta ambazo zinatumia fedha nyingi sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Ukiangalia *component* ya bajeti katika sekta ya ujenzi *in its totality* ni fedha nyingi sana. Baraza la Ujenzi ni la muhimu sana kwa sababu ndilo ambalo inabidi liangalie hali ya sekta hii ya ujenzi. Sasa ukiangalia hapa watu wengi tunadhani kazi ya *NCC* ni ya *CRB*, ni kazi ya wale *architects*. Kazi yao ni tofauti kabisa. *Permanent objective* ya *CRB* ni *contractors registration board* ni kuwarejista *contractors* tu. Lakini hawa *NCC* wanakwenda mbali zaidi, kazi yao kubwa namba moja ni ku-*provide leadership* katika sekta ya ujenzi.

Kwa mfano, tunayo matatizo ya *technology changes*, nani anahangaika nayo? Dunia ya leo mabadiliko ya teknolojia ni makubwa sana, nani anaishauri Serikali katika mabadiliko ya teknolojia kwamba ni wakati gani sasa tutumie teknolojia ipi? Nani anaishauri? Ni *CRB*, *ERB* au ni nani? Hapa ndipo inapokuja nafasi ya Baraza la Ujenzi. Lakini pia ziko *unit price* za ujenzi wote, gharama za ujenzi nani anazi-*analyse* kusema hivi kweli gharama hizi tunazotumia ni sahihi ama sio sahihi?

Nani anafanya kazi hii? Anayefanya hii kazi kwa vyovyote vile ni Baraza la Ujenzi. Baraza la Ujenzi linatakiwa liende hata kule Wazo *Hill* likachukue *informations* kujua hivi kwa nchi Watanzania tunahitaji labda saruji kiasi gani? *Trend* yetu kwa miaka 10 ni nini? Hizi ndizo kazi za Baraza la Ujenzi. Mimi ninachosema chombo hiki kwanza kinatakiwa kiongezewe nguvu ili kiweze ku-*provide* hii *information* kwa kuishauri Serikali ili tuweze kwenda vizuri zaidi kulingana na mabadiliko ya dunia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ambacho kilikuwa kinanisumbua ilikuwa ni *section 4* ambayo bahati nzuri imekwishafanyiwa *amendment* kwamba zile *dissemination information* kuwe kuna *one centre* na bahati nzuri tuna *CRB*. Kwa *CRB* wakisha *register* hao *contractors* wao wote wakimaliza wapeleke zile *information* kwa watu wa *NCC*.

Mimi hilo sina tatizo nalo kabisa ambalo lilikuwa linanisumbua mwanzoni ni hilo la kutaka kwamba mtu mmoja apeleke *information* kwenye Bodi mbili. Kwa hiyo, kwa sasa kwa mabadiliko haya watakuwa wanachukua *information* kwenye hivyo vyombo. Wizara ya Ardhi wameanzisha bodi zao na zile bodi lazima nazo hawa *NCC* wakachukue *information* kule. Kwa hiyo, kazi ya *NCC* ni kubwa zaidi ukiangalia *in a bigger picture* katika sekta ya ujenzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *section 4K* inasema: “*Manage the fund for training of personnel in the construction industry.*” Waziri atakapofanya *amendment* kama atakubaliana na mimi ningetamani isomeke: “*Establishing and managing the fund for training of personnel in the construction industry*”. Hivi ndivyo ningependa ingesomeka na sio *to manage to established* kwa sababu hiyo *fund* haipo.

NAIBU SPIKA: Rudia maneno yako basi!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Nasema *section K* hii inasema: “*Manage the fund for training of perssonel in the construction industry*” lakini hiyo *fund* tunavyoongea sasa haipo. Kwa hiyo, nikawa nashauri tui-*re-phrase* tuseme: “*Establishing and managing the fund for training of personnel in the construction*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema hii sheria imekuja kwa wakati, umefika wakati sasa watu wa *NCC* waende mbali zaidi kuweza kupata hizi *information* vizuri na kuzi-*analyse* na kuonyesha *trend* ya sekta ya ujenzi katika nchi yetu. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. VITTA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia Muswada huu wa Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi wa Mwaka 2007 (*The National Construction Council Amendment Bill, 2007*). Nami naomba niungane na wenzangu kuanza kuupongeza Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuchagua viongozi wetu wa Chama chetu cha Mapinduzi kwa kumpa kura nyingi Mwenyekiti wa Chama chetu na Makamu wake wote wawili kura za vishindo na kwa kuwachagua Wajumbe wa Halmashauri Kuu. Pia nawapongeza Wajumbe wa Halmashauri Kuu kwa kuwachagua Wajumbe wa Kamati Kuu na Sekretariat na kumpata Katibu wetu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila, naomba nitumie fursa hii kwa dhati kabisa inayotoka ndani ya moyo wangu kwa kuwashukuru Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kwa kumchagua Bi Zainab Kawawa kwa kura za kutosha. Nawashukuru sana, ahsanteni sana! Naomba nianze kwa kusema naunga mkono Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria hii. Lakini nianze pia kwa kuungana mkono na Mzee Mzindakaya kwa yale aliyosema tuwape uwezo makandarasi wadogo ili waweze kupata vifaa vya kufanyia kazi za ujenzi hususan wa barabara. (*Makofi*)

Nasema hivi kwa sababu sisi kwa mfano kule kwetu Mkoa wa Ruvuma, makandarasi wetu huwa wanapata taabu sana kwa sababu hawana uwezo. Ulifika wakati iliwabidi lazima wakakodi vifaa nje ya Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, huwagharimu sana kupata kifaa kutoka kama Dar es Salaam, lazima ukisafirisha kwa gharama yako. Kama ni Mtwara lazima usafirisha kwa gharama yako kupeleka kwenye *site* yako ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi tuna mmoja ambaye ana vifaa lakini yeye hatoshi na kwa ajili ya uchungu wa makandarasi wadogo walioko Mkoa wa

Ruvuma akaamua kuuza nyumba yake iliyopo Dar es Salaam ili kununua vifaa vya ujenzi wa barabara ndivyo kidogo vinatusaidia katika Mkoa wa Ruvuma. Mtu mwenyewe si mwingine ni Mzee Mustapha Mohamed Songambele kwa uchungu wa maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma aliuza nyumba yake akanunua vifaa. Hivyo nilikuwa nataka kuuliza hapo zamani tulikuwa na vituo vilivyokuwa chini ya iliyokuwa inaitwa *Public Works Department (PWD)* ambayo jina maarufu wakati huo ilikuwa inaitwa “Punda Wengi Duniani”. Ilikuwa inaweka vifaa vya ujenzi vya barabara katika vituo hivyo ambavyo ilikuwa inasaidia kutengeneza barabara zetu za vumbi wakati zinapoathirika na mvua hususan na mvua.

Nilikuwa nauliza sheria ya kuwa na vituo vile imefutwa au ipo? Je, Serikali inaweza kuweka utaratibu wa kurudisha angalau vituo hivyo vikawepo ili makandarasi wetu wadogo wakapata uwezo wa kukodisha kwa urahisi zaidi katika maeneo yale husika?

Mheshimwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi inanikumbusha wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Wilaya ya Tunduru ulikuwa wakati wa masika. Tulipata shida sana hasa barabara kubwa ambazo zilikuwa chini ya *TANROADS*. Ulifika wakati unasafiri kwenda kufanya kazi ya Kampeni unakuta barabara imeharibika, imefungwa, vijana wametengeneza barabara yao wamekata miti, wamepanga miti na ukitaka kupita katika barabara yao hiyo ni lazima ulipe hela shilingi elfu tano.

Lakini kwa nguvu waliyopewa Mheshimiwa Waziri Mkuu tulimshukuru wakati ule aliagiza *TANROADS* waweze kurekebisha barabara hiyo na vifaa hivyo vilibidi vifuatwe Mtwara kwenye barabara inayotengenezwa ya Lindi/Mtwara kuja Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunalishauri Baraza hili kuwa sheria hiyo ya kuwa na vituo vya ujenzi wa barabara au vituo vya ukodishaji vifaa vya ujenzi wa barabara vingekuwapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi, mchango wangu ulikuwa ni huo, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuupongeza muswada huu na marekebisho yake yote. Ningependa kujua *consequences in case NCC does not perform its duties*. Naomba nijibiwe. Endapo chombo hiki hakitekelezi majukumu yake kama ilivyokusudiwa kwa maana ni chombo muhimu sana ambacho kilikuwepo lakini msaada wake umekuwa mdogo katika nchi. *So what are the consequences in case NCC does not perform its duties and responsibilities*. Baada ya ufafanuzi huo naunga mkono na naomba kuwasilisha.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho kwa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hoja ambayo nimeiwasilisha jioni hii. Nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii na wamechangia kwa ufasaha sana, nawashukuruni sana. Nianze na wale waliochangia kwa maandishi, nao ni: Mheshimiwa William Shellukindo,

Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. Waliochangia kwa kusema humu Bungeni ni Mheshimiwa Felix Kijiko, amechangia kwa niaba ya Kamati ya Kudumu na mwingine alikuwa Mheshimiwa Shamis Bakar Faki, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Peter Serukamba na mwisho kwa kutaja lakini sio kwa umuhimu ni Mheshimiwa Vitta Kawawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na moja la jumla tu kuhusiana na chombo chetu cha NCC. Mengi yamesemwa ni chombo kikongwe na hiyo sheria ilitungwa mwaka 1979 lakini wale ambao tunakumbuka hakikuanza kazi rasmi mpaka mwaka 1981 kwa lengo zuri tu la kuanza maandalizi ya kazi. Tunampongeza sana *Engineer* Msita amefanya kazi ya uhakika sana katika kukilea chombo hiki. Yawezekana chombo hiki kwa wengi hakifahamiki sana kwa sababu hakina mtandao mikoani. Lakini nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa kipindi chote hicho chombo hiki kimefanya kazi nzuri sana. Kimekuwa chombo cha msaada mkubwa sana kwa Serikali katika sekta ya Ujenzi. Kimeendesha mafunzo ya aina mbalimbali kwa makandarasi na wadau mbalimbali hapa nchini. Ni chombo hiki kilichopendekezwa uanzishwaji wa hizo Bodi tatu ambazo mnasema na zenyewe zimefanya kazi nzuri.

&&&

NCC ndiyo imependekeza uanzishwaji wa Bodi ya Wasinifu Majenzi au Majengo na Wakadiraji Majengo. Chombo cha Usajili wa Wahandisi kilikuwa ni hawa. Chombo cha Usajili wa Makandarasi kilipendekeza NCC kwa sababu waliona mbele kwamba taaluma hizi na kwa miradi ambayo wanaifanya unahitaji ukawa na usimamizi ulio bora na unaupata kama unakuwa na utaratibu wa kusajili, unawajua hao na unasema wewe huwezi ukasimamia kazi hii iko juu ya uwezo wako, *sorry*.

Sasa hawa ndiyo walishauri hayo na Serikali ikaitika mwaka 1997 tukatunga sheria hizo. Lakini hawakuishia hapo, NCC ndiyo imeshughulikia uanzishwaji wa Taasisi mbalimbali za kitaaluma, kwa mfano, *The Architects Association of Tanzania, The Tanzania Institute of Quantity Surveyors, The Association of Consulting Engineers Tanzania, The Tanzania Civil Engineering Association, The Tanzania Roads Association* na *Tanzania Institute of Arbitrators* yaani Taasisi ya Usuluhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kimefanya mazuri, wamo lakini hawavumi na pia mimi kama Mwanasheria Mkuu Mstaafu wa nchi hii najua wametusaikia sana katika baadhi ya migogoro ambayo tumekuwa nayo. Wamejenga uzoefu wa kina sana katika masuala haya na bado wanatumika na makandarasi ambao wanakuwa na migogoro.

Sera ya Ujenzi ambayo tuliileta Bungeni humu ilipendekezwa na kufanyiwa kazi na chombo hiki na sisi Wizarani walipoileta tukaizamia ndiyo tukaikumbatia tukapata nguvu ya kwenda Serikalini na hatimaye kuja Bungeni. Wamefanya kazi ya ukaguzi wa kiufundi tunaita *Technical Auditing* ya miradi mbalimbali yenye thamani kubwa kwa

sababu wana uwezo hawa na wale ambao mnaipenda sana Sekta ya Ujenzi nchini mnajua majarida yao ambayo wanayachapisha *from time to time*. Kabla ya kutunga Sheria ya Manunuzi ya Umma, Kanuni ambazo zilikuwa zinatumiwa kabla ya Sheria hiyo na Kanuni hizo ziliasisiwa na chombo hiki.

Kwa hiyo, ndugu zangu mimi nasema tunaweza tukawa na mambo mengine lakini hiyo si hoja, hoja ni ile aliyosema Mheshimiwa Peter Serukamba. Nawaombeni ndugu zangu myasome maudhui ya majukumu ambayo yanapendekezwa kupitia Muswada huu. Ni majukumu mazito kwelikweli! Sawa unaweza ukasema kama alivyonihauri Dr. Nkya kwamba kutunga Sheria *is one thing* kuitekeleza *is another thing*. Sawa mimi sina tatizo hilo. Lakini nataka niwaambie tumedhamiria kweli chombo hiki tukiimarisha, tunakiimarisha kupitia kuomba fedha ya Bajeti, tunachukua ushauri wa Kamati ya Bunge ya Kudumu kwamba labda tufikirie tuwe na *skills and development levy*. Lakini hapa ni ninyi Waheshimiwa Wabunge mmekuwa wa kwanza kututahadharisha kwamba tunawaumiza wadau na tozo nyingi hizi mkasema hamuwezi mkafikiria njia muruwa ambayo inawapatia fedha za kutosha kufanya shughuli zao.

Sisi tutaendelea kwa sasa kuja Bungeni na kuomba fedha lakini *functions* hizi ndizo zenyewe, *to promote and provide strategic leadership for the growth development and expansion of the construction industry in Tanzania with emphasis on the development of the local capacity* kama alivyosema Mheshimiwa Mzindakaya *for social economic development and competitiveness in the changing global environment*. Kwa sababu lazima twende na wakati, sekta ya ujenzi nchini ipende isipende lazima ikubali kukumbatia teknolojia ya kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na yapo mengi ambayo yametajwa humo. Sasa ukiondoa hicho kifungu cha 4 (f) ambacho nitakisemea kwa kifupi baadae, mengine haya ni mazuri na ni ya msingi na pale aliposema Mheshimiwa Serukamba kwenye (k) ndiyo maana sisi kwenye *schedule of amendments* tumesema chombo hiki *ki-solicit*, yaani kwenda kutafuta fedha na wakipata *ku-manage* wazisimamie fedha hizo za mafunzo katika kujenga uwezo wa wadau katika sekta ya ujenzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe radhi sana kumchanganya rafiki yangu Abbas Jecha na Bakari Faki. Aliyesimama na kusoma hapa ni si Mheshimiwa Bakari Shamisi Faki bali alikuwa ni Mheshimiwa Abbas Jecha. Samahani sana!

Hilo nadhani ni la msingi sana katika kulipatia upeo wa chombo hiki. Sasa lipo jingine hili la usajili. Kama ilivyoielezwa humu hivi vyombo vitatu, hizi Bodi tatu *CRB, ERB* na *AQRB* ni vyombo vya usajili. Kwanza, vinashughulikia taaluma lakini pia vinasajili miradi ya Wahandisi na miradi ya Wabunifu Majengo na wakadiriaji majengo wanaofanya kazi hizo na lengo la Sheria hizo tatu ni kuhakisha kwamba kazi zinazofanywa na wanataaluma hao na Makandarasi hao kweli ni wale wenye sifa na uwezo wa kazi hizo kisheria. Sasa kwa makundi haya matatu maana kwanza ni *professions* hizi wanajisimamia wao na kujidhibiti wao na ndiyo suala zima la maadili ambalo alikuwa analisema Mheshimiwa Lucy Nkya inaingia. Ukitetereka katika kazi yako, katika maadili yako unashughulikiwa na ndiyo maana wao kule wako macho sana,

tunashukuru upungufu uliokuwepo huko nyuma na nilisema majuzi baadhi ya marekebisho tuliyoaleta hayo hasa kwa upande wa *Engineers Registration Board* na tutakuja *Contractors Registration Board* na tutafika kwa upande wa *Architects and Quantity Surveyor Registration Board*, yanatokana na mapendekezo ya ripoti ya Kamati aliyoiunda Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na lile jengo la Chong'ombe kuporomoka pale.

Wameleta mapendekezo mazuri, sasa yapo mengine kwa sababu tuliwahi kukimbia kuwapeleka mahakamani ndiyo maana nikasema *process* ya Kimahakama sisi kama Serikali hatuna uwezo wa kuwaambia leo amueni, mfungeni huyu! Hatuna tunaziachia mahakama uhuru huo zifanye. Lakini haya ambayo tuliyaona yana upungufu ndani ya Sheria hizi ndiyo tunayaleta haraka yashughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4 (f), mkiyasoma yale marekebisho tuliyoasilisha, mtaona kabisa kwamba tumejaribu kuyaweka katika mtiririko ambao hauleti mkanganyiko kama alivyoeleza Mheshimiwa Mnyaa. Vyombo vya Usajili wa miradi tunataka vibaki kuwa ni hivi vitatu na vingine tunajua viko kwenye Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, vipo vyombo hivyo. Sasa tunasema kwa usajili na usajili *is a formal process*, maana unaomba katika utaratibu uliowekwa, wanakupima kama una sifa hizo, wakiona unazo wanakusajili, wakiona una upungufu wanakwambia ahsante, hapana, subiri bwana fanya haya na haya. Ndiyo maana *wording* ambayo inapendekezwa kwa *NCC* itakuwa ni kuweka orodha ya miradi. Sasa wao wanapataje taarifa hizo? Ndiyo marekebisho ambayo yameletwa kupitia ibara ya saba.

Ndiyo yanajibu hoja hiyo watakaotakiwa kutoa taarifa hizo ili hawa wazipokee na *kuzi-compile* na *ku-list* kwa maana ya moja, mbili, tatu na majina mpaka unakamilisha wametajwa hapa, (a) ni wale ambao wanajishughulisha na shughuli za ujenzi; (b) ni kundi la hawa watatu, hizi bodi na zile za ardhi na wengine ambao watakozaliwa. *Performing function of registration of personals engaging or intending to engage in any activities of the construction industries*. Na wenyewe hawa ndiyo wanatakiwa wakiwezeshe chombo hiki kupata taarifa hizi kwa shughuli zao ili watekeleze majukumu ambayo tumeyainisha katika kifungu cha nne. Kwa hiyo, hakuna mkanganyiko pale, sasa suala la kutoza faini hutozwi faini kwa sababu eti wewe husajili, hapana! Unawatoza faini hawa kwa sababu wanatakiwa wakupe taarifa hizi. Kwanza kwa vyombo vya Serikali hatutegemei kwamba Bodi hizi zitakaidi maana miradi ile wanayo, na wameisajili lakini kuondoa ile *doubt* na kuleta uwazi katika suala hili ndiyo tumeanisha hivyo lakini akikaidi na yeye wanamnyoa ndevu. Ndiyo kifungu hicho Mheshimiwa Mnyaa kina lengo la kuweka bayana suala hili kwamba ni *mandatory* kwa taarifa hizi.

Hakikufungi chenyewe, unafungwa na Mahakama, ukipatikana na hatia sasa ndiyo unakuja ile faini. Hapa nakubaliana na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo katika mchango wake ni sahihi kabisa *not exceeding*, ukiweka hiyo huji mara kwa mara Bunge, na ndicho tulichokifanya ukisoma kifungu cha 12 cha Sheria mama. Maneno yaliyomo kwenye Sheria ni *not exceeding*, sasa zile kiwango cha faini kimepitwa na wakati kwa sababu ilikuwa mwaka 1979 na hatujalitembelea eneo hili sasa ndiyo tunalitembelea. *Not exceeding 500,000/= shillings and not exceeding 1,000,000/=*. Kwa

hiyo, tunakuja kwa upeo mzuri ambao mwenzetu alikuwa ameuona, tumeuona wote katika mtazamo huo.

Kwa hiyo, mkanganyiko kati ya kifungu cha 4 (f) na 7 (a) haupo. Namshukuru sana Mheshimiwa Mzindakaya maana mafunzo ya nadharia, mafunzo ya vitendo ndiyo yanakamilisha uwezo wa taasisi na uwezo wa mtu, uwezo wa Makandarasi. Ndiyo maana hata vyombo hivi vitatu na wenyewe wana mafunzo kwa wanachama wao. Lakini hawa wanaiangalia *Construction Industry* katika upana waka na ndiyo na wenyewe wana kazi hiyo. Sasa suala hilo la makandarasi wazalendo, wazawa ni suala ambalo limekuwa linajitokeza sana, hawana mitaji, hawana vifaa, wanafanya nini, yote hayo. Ni kweli ndugu zangu lakini jamani tumepiga hatua kidogo. Mkisoma taarifa juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alitupa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika shughuli yetu ya *CRB* katika kutimiza miaka kumi tangu ianzishwe.

Taarifa ya mwaka au taarifa yao waliyoitoa kwa kazi ambazo walizifanya kwa kipindi cha miaka kumi na moja ambalo linajitokeza kwa wazi ni kwamba kazi za sekta ya ujenzi nchini, ukichukua mgao wa soko, ile *market share* kati ya makandarasi wa nje na wa nyumbani imekua. Ilianza sifuri ikapanda asilimia moja sasa tumefika asilimia thelathini. Si haba na huko tunakokwenda ushindani utakuwa mkali sana hasa tutakapoingia tukawa Shirikisho la nchi za Afrika Mashariki, hata kabla ya kufika kule ushindani huu ni lazima na sisi tujipange vizuri sasa tunafanya nini katika kuwezesha hawa. Wiki ijayo naamini Serikali itawasilisha Muswada Bungeni unaoshughulikia masuala ya *lease financing*. Niliieza majuzi *lease financing* ndiyo njia mojawapo ya kuwawezesha hawa makandarasi na walandisi ambao wanataka kuzifanya kazi hizi waweze kwenda kupata mkopo kutoka kwenye Mabenki ambayo yatafanya kazi hii. Unawezeshwa kwa kukopa, unalipa kutokana na malipo unayolipa unapofanya kazi lakini hayaji kwako moja kwa moja lakini yanalipwa kwa yule aliyekukodishia mitambo na vifaa vya kazi.

Kipindi cha kukodi mitambo kikiisha una *option* ya kununua mitambo hiyo, lakini pia kuna *option* ya kutokuinunua usipochukua chaguo lako hilo la kuinunua basi wao wanaendelea kuitoa kwa wengine. Hii ndiyo itasaidia sana kujenga uwezo wa Makandarasi wetu ili na wenyewe waweze kuhimili ushindani. Lakini Serikali kazi yake ni kutengeneza fursa, inatoa mazingira haya yawe yako pale, Serikali haiwezi ikawalazimisha hawa kushiriki. Sasa fursa ni kwa wale wanaotaka kuzitumia lakini naamini ni changamoto iliyopo kwa wazalendo wetu hawa wadogo waweze kupata vitendea kazi na mitambo na zana mbalimbali za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu ya kwanza yale kuhusiana na kazi inayofanywa na *NCC* pamoja na haya ambayo yamo kwenye muswada, yale aliyoyasema rafiki yangu Mheshimiwa Mnyaa kwamba *NCC* imepitwa na wakati, nadhani na yeye anakubaliana na mimi kwamba chombo hiki hakijapitwa na wakati. Pili, chombo hiki hakiwezi kufanya kazi ya sera, sera inatungwa na sera. Vyombo hivi ni vya kutekeleza sera za Serikali kwa suala zima la ujenzi. *CO* ateuliwe na Waziri sawa, lakini baada ya kushauriana na vyombo husika. Sasa hivi Mheshimiwa Rais alikuwa anamteua huyu kwa kushauriana na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu, kwa sababu nategemea Waziri yeyote mwenye dhamana ya masuala haya atathamini ushauri anaopewa na vyombo vyake na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekuwa akishauriana na Wizara kuteua mtu mwenye sura inayofanana na Sheria na tutendelea kufanya hivyo. Uamuzi wa kutomhusisha Mheshimiwa Rais si kwamba nafasi hii ni ndogo hapana, la hasha! Mheshimiwa Rais ana kazi nyingi mno, tukasema angalau kazi zile na hawamfahamu yeye hawa, sisi tunawafahamu kwa sababu tunashinda nao na tunahangaika nao, kila siku inakuwa rahisi kuliona kwa haraka kwamba fulani anafaa atatusaidia katika hili.

Limeletwa suala la Hoja *mainstreaming* ya *gender* kwenye Bodi ya NCC. Tutaliangalia namna gani kufanikisha suala hili. Ni hoja ambayo nadhani inaenda na wakati tu wa sasa. Nyakati tulizonazo hizi zimekuwa za madai mengi ya namna hii na mengine yanayofanana na dai kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa William Shellukindo amesema jamani iwe *mandatory* kwa anayejenga nyumba, haya maghorofa maegesho inakuwa kero. Jengo linakuwa zuri kubwa lakini hakuna *parking*. Sasa huu ni ushauri wake tunauchukua ili tulifanikishe hili tunahitaji kushirikiana sisi wa miundombinu, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Kwa hiyo, sisi tunalichukua na tunaliona ni kero kweli kweli labda ni Tanzania tu ambapo tuna taratibu hizi. Lakini nchi nyingi wewe ghorofa ya kwanza ya pili ni chini na tatu ni *parking* kama walivyofanya wenzetu wa *PPF Tower*, *JM Mall* na wengine wanaofanya kazi kama hizo. Kwa hiyo, tunauchukua ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa hayo mengi ambayo yalikuwa yamesukumwa kwa nguvu nimeyagusa. Kama sikuyagusa basi yawezekana na mimi sikuwa nasikiliza mchango wa Waheshimiwa Wabunge. Lakini waniwie radhi natumaini nimejaribu kuya-*capture* karibu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea yale ya ushauri hasa ambayo yapo kweye ripoti ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu.

Yapo maeneo mazuri tu ambayo tunayachukua na yale mengine ambayo yametokana na Waheshimiwa Wabunge waliochangia sasa hivi tutaangalia namna ya kuyashughulikia. Lakini ni ushauri mzuri tunathamini sana mchango huo na baada ya kusema hayo nimalizie kwa kusema nawashukuru sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 (*The National Construction Council Amendment Bill, 2007*)

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 7

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 7 ningeomba ufafanuzi. Ni kweli kimererekebishwa tena na kifungu cha 7(1)(a), kuna ile *performing the function of registration* kwamba hizo Bodi za *CRB, ERB* ndiyo wanapaswa ku-*furnish information* kwa *NCC*. Lakini pia katika (a) kuna ile *every person who is engaged or intending to engage* na hapa pia imezungumza kwamba ana-*furnish information* kwa *NCC*.

Nataka Mheshimiwa Waziri atufafanulie ikiwa huyo *person* anayekusudia kama ni *investor* ambaye *investor* huyu ame-*furnish information* kwa *Investment Committee* halafu *TRA* na vilevile a-*furnish information* kwa *NCC*.

Halafu kuna kifungu hapo hapo cha *penalty* kama haku-*furnish information*; je, kwa nini na wakati huo huo kifungu (f) kimefutwa cha usajili na hawa *CRB* na *ERB*

ambao wanasajili ndiyo wana hizo *provision za penalty*? Hawa sasa kwa nini bado wawe na kifungu cha *penalty* wakati hawasajili? Naomba ufafanuzi na huyu ni mtu binafsi na ameshapeleka *information* kwenye hizo Bodi nyingine.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa maelezo yangu, ni vizuri Mheshimiwa Mnyaa tukaenda kwa kituo hatua kwa hatua ili alielewe.

Kwanza tukianza na taarifa zinazopelekwa *TIC*, mtu anapokuja kama Mwekezaji hapa, anasema mimi nataka kulima mpunga Bukene nitafutieni eneo, *TIC* wanamtafutia hizo taarifa sisi haziingii katika *construction industry*. Kama anataka kuja kuwekeza katika ujenzi re-estate ile itampa tu yeye utambulisho tu kule ili aweze kupata vile vivutio kama Mwekezaji.

Sasa atakapoanza ile shughuli yenyewe iliyomleta kujenga zile nyumba za makazi ama za ofisi, kwanza lazima aanze hatua ya kwanza ya usanifu maandalizi ya eneo hilo, hawa wataalamu ni nani anayefanya kazi hiyo. Sisi tunamtaka sana huyo. Akiwa ni msanifu wa majengo mradi huo ni mkubwa kiasi gani tunataka tumwelewe kama kweli kazi hiyo kwa sifa alizonazo anaweza akasimamia mradi huo.

Sasa hiyo ni kazi ya Bodi ya *Architects and Quantity Surveyor Registration Board*. Itakapokuja hatua sasa ya kwanza wanafikia sasa shughuli yenyewe ya kuanza kujenga nani anayepewa kazi hiyo ya kama mkandarasi ni wa *class* gani. Kwa sababu ukubwa wa mradi lazima uendane na *class* ya mkandarasi na vilevile Mhandisi anayesimamia mradi huo.

Ndiyo maana kile kibao kinachowekwa kwenye *site* ile ya ujenzi kinataja wale watu wahusika muhimu sana kwa Bodi hizi tatu kwa sababu ndiyo unataka wafuatilie hawa jamaa wanaingia tu pale kujitambulisha. Hebu onyesha orodha ya wafanyakazi *key personal* ambao wanasimamia mradi huu. Kama kuna upungufu wanakwambia kesho uje ofisini. Sasa hiyo ndiyo tunasema shughuli ambayo itaendelea kubaki kule.

Lakini *NCC* kwa sababu ya *functions* ambazo zimetajwa katika kifungu cha 4 wanazihitaji taarifa hizi na wenyewe kwa kazi zao. Sasa wazipataje kwa kwenda kuwapigia watu magoti? Hapana! Sheria iruhusu zipatikane. Kundi la kwanza ni huyo huyo ambaye unamsema amekuja kufanya kazi ya *Re-estate*, ana mradi wake.

Kwa hiyo, taarifa hiyo anatupeleka kujua tu kwamba si ku-*register* hapo *NCC* hawasajili, wao wanaorodhesha kwamba kuna mradi uko maeneo ya Kibaha au Bukene au wapi. Tukienda kwa namna hiyo unanza kuona. Sasa suala la faini pale linakuja tu kwamba hatua ya kwanza umekaidi kupeleka taarifa hizo katika ngazi ya huyo mwekezaji wako, ngazi ya pili ni Bodi ya Serikali ambayo inawasajili hawa, ameshindwa kupeleka taarifa hizi. Sasa ndiyo maana imeandikwa kwa ufasaha zaidi kuweza kukidhi sura hizo zote mbili.

Lipo lingine ambalo mpaka uisome Sheria mama yenyewe Bodi au Baraza hili linaweza likataka lipewe taarifa zingine, ukikaidi ndiyo unakuja kwenye kifungu kile ambacho tumeongeza sasa faini inakuwa sio shilingi 15,000/= inakuwa isizidi shilingi milioni moja. Sasa yote haya yana maana yake; umekaidi kutoa taarifa ambazo Mamlaka iliyotakiwa na Sheria uipatie wewe hukufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiliona katika mtazamo huo wala hakuna kitu ambacho kinaharibika. Nakushukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na Marekebisho yake)*

(Bunge lilirudia)

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa
(The National Council (Amendment) Bill, 2007)**

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 *(The National Construction Council*

(Amendment) Bill, 2007) Kifungu kwa Kifungu pamoja na marekebisha ambayo yamefanywa na kuukubali.

Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hatuna matangazo yoyote, kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 1.13 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 9 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*